# Nipashe

Ijumaa Oktoba 23, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580377

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



FURSA

Mawakala na wasambazaji wa uuzaji Magazeti

Kwa Maombi na Ufafanuzi zaidi Wasiliana nasi

Meneja Usambazaji na Masoko
Mikocheni Light Industrial Area
S.L.P 31042,
Dar es Salaam,
Tanzania

Namba :+255716500500
Barua Pepe:circulation@guardian.co.tz
Mwisho wa Maombi ni 27 Oktoba 2020


**BIBI** mbaroni tuhuma za kukeketa kitoto kichanga cha siku 9

UKURASA 3



**BIL.** 136/- zatengwa kukarabati viwanja vinne vya ndege

UKURASA 3

# JPM atoa ahadi 10 Jimbo la Hai




**ZIMO** migogoro ya ardhi, barabara za lami, maji, ufufuaji viwanda na maslahi bora kwa wafanyakazi... *Endelea Uk. 2*



Mgombea urais kupitia CCM, Dk. John Magufuli akizungumza na wananchi katika mkutano wa kampeni uliofanyika Bomang'ombe, wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: IKULU**

# Lissu aahidi Muungano wa usawa pande zote

UKURASA 2



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Seif Sharif Hamad (kulia), akimnadi mgombea urais wa Tanzania kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, katika mkutano wa kampeni kwenye viwanja vya Tibirinzi Pemba, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**WENYE KIGUGUMIZI WATOA TAMKO ZITO**

WATU wenye kigugumizi nchini, wameadhimisha siku yao jijini Dar es Salaam, huku...

**Marekani yaeleza msimamo uchaguzi**

UKURASA 2

**MICHEZO** KMC YATANGULIA MWANZA KUISUBIRI YANGA JUMAPILI UK. 23

**MAONI, KATUNI UK. 6**

HABARI KITAIFA

# Bibi mbaroni tuhuma kukeketa kichanga

**Na Richard Makore,**
MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza, linawashikilia watu wanne kwa tuhuma mbalimbali likiwamo la kukeketa mtoto wa siku tisa pamoja na kukutwa na kadi 49 za kupigia kura za watu wengine.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne Muliro, akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, alisema Getrude Felician mkazi wa kijiji cha Chibasi wilayani Ukerewe, alikamatwa kwa madai ya kumkeketa mjukuu wake (jina linahifadhiwa).

Muliro alisema mtuhumiwa huyo ambaye ni bibi wa mtoto huyo, anadaiwa kutenda unyama huo hivi karibuni na kumsababishia mtoto huyo kutokwa damu nyingi.

Alisema mtuhumiwa hiyo anashikiliwa na Jeshi la Polisi na kwamba muda wote atafikishwa mahakamani.

Katika tukio lingine, alisema watu watatu walikamatwa wilayani Magu mkoani Mwanza wakiwa na kadi 49 za kupigia kura kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Shida Kitwanga, Peter Malemi na Kulwa Patrice wote wakazi wa Magu.

Kamanda Muliro pia alisema Deogratias Medard alifariki dunia baada ya kudaiwa kula chakula chenye sumu wilayani Sengerema.

Kuhusu uchaguzi mkuu, Kamanda Muliro alisema wamejipanga vizuri ili kuhakikisha kila mtu mwenye sifa anapata fursa ya kupiga kura bila hofu yoyote.

# Bil. 136/- kukarabati viwanja vya ndege

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 136 kwa ajili ya ukarabati mkubwa katika viwanja vya ndege vilivyoko mikoa ya Kagera, Rukwa, Shinyanga na Kigoma.

Katika hafla ya uzinduzi wa kuanza kwa mchakato huo jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, alisema ukarabati huo umelenga kuvifanya viwanja hivyo kuwa na ubora wa kimataifa.

Alisema miongoni mwa mambo ambayo yatazingatiwa katika uboreshaji wa viwanja hivyo, ni pamoja na kuongeza maeneo ya maegesho ya magari, kuongeza urefu na upana wa viwanja, kujenga mitambo ya taa yenye alama za kuongoza ndege, kuweka mifumo ya majitaka, kukarabati majengo ya abiria na kujenga uzio mkubwa kuzunguka viwanja kwa ajili ya usalama.

Katibu aliongeza kuwa hawatokuwa tayari kupokea ombi la kuongeza muda kwa ajili ya kukamilisha mradi, hivyo akawataka wasimamizi waliopewa kazi hiyo kuzingatia muda.

"Niseme tu ukweli serikali hii ipo macho sana, kwa hiyo pesa zipo, fanyeni kazi usiku na mchana, hatutataka kisingizio chochote, tunataka kazi ikamilike kwa muda uliopangwa. Kuna viwanja kama Kagera na Kigoma tumetoa miezi 12, ikifika hiyo miezi kila kitu kiwe tayari na watu waanze kupata huduma.

"Lakini kwa kiwanja cha Sumbawanga na Shinyanga tumetoa miezi 18, ukifika huo muda watu wakabidhi kazi ili wananchi waendelee kunufaika na huduma, serikali hii haina mchezo," alionya.

James alisema kukamilika kwa viwanja hivyo kutaongeza ajira, pato la ndani, biashara, kukua kwa sekta ya utalii nchini na kuongeza mianya ya ufanyaji biashara.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Patrick Mfugale, alisema lengo kubwa la kuvifanyia maboresho viwanja hivyo ni kuhudumia ndege kubwa kama Bombardier na Airbus.

"Tunavitanua na kuviongezea urefu viwanja hivi vya ndege ili tuweze kuhudumia ndege kubwa ambazo mwanzo zilikiwa hazitui hapa kwa sababu viwanja hivi havina ubora wa kimataifa wa kuruhusu ndege kubwa kutua," alisema.

Akiongea kwa niaba ya wakuu wa mikoa ambao mradi huo unaokwenda kufanyika, Katibu Tawala Mkoa wa Kigoma, Rashid Mchatta, alipongeza serikali kwa jitihada hizo.




TANGAZO

# TPB BANK PLC

Tpb Bank
Grow with us

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA(HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### TPB BANK PLC
### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2020
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | | |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 38,188 | 40,992 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 56,064 | 18,055 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 143,224 | 154,108 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 32,887 | 32,757 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 208 | 1,333 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 82,313 | 86,046 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 627,499 | 603,218 |
| 12 | Mali Nyingine | 63,305 | 65,686 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 22,285 | 24,347 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,065,973** | **1,026,541** |
| B | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 700,578 | 708,263 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 66,047 | 47,340 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 4,664 | 3,463 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 85 | 110 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 20,138 | 18,708 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 2,671 | 2,581 |
| 27 | Dhima Nyingine | 20,836 | 21,971 |
| 28 | Madeni | 124,336 | 102,304 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **939,354** | **904,740** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **126,619** | **121,801** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28,072 | 28,072 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 60,601 | 60,601 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 13,214 | 8,396 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 24,732 | 24,732 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **126,619** | **121,801** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 0 | 0 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 94,642 | 98,855 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 36,361 | 36,191 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 38 | 52 |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11.88% | 11.87% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 13.88% | 15.04% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 97.31% | 92.77% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 58.87% | 58.76% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79.51% | 64.59% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -1.09% | 57.60% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 3.84% | 56.11% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
### KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2020
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 30/09/2020 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30/09/2019 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/09/2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30/09/2019 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 35,163 | 25,949 | 89,420 | 75,462 |
| 2 Gharama za Riba | (11,474) | (6,026) | (27,495) | (15,881) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **23,689** | **19,923** | **61,925** | **59,580** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (37) | (298) | (359) | (725) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (793) | (3,375) | (5,328) | (8,091) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **6,486** | **7,498** | **20,896** | **20,057** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za | 1,799 | 873 | 3,741 | 3,296 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 4,012 | 4,256 | 10,660 | 10,475 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 674 | 2,369 | 6,495 | 6,286 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(22,827)** | **(17,580)** | **(58,673)** | **(53,242)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 11,048 | 7,935 | 28,479 | 24,621 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 1,264 | 996 | 3,744 | 2,867 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 10,516 | 8,649 | 26,449 | 25,753 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **6,518** | **6,168** | **18,462** | **17,579** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 1,700 | 1,725 | 5,249 | 5,175 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **4,818** | **4,443** | **13,214** | **12,404** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **4,818** | **4,443** | **13,214** | **12,404** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 1,049 | 886 | 1,049 | 886 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 172 | 158 | 471 | 442 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 44 | 36 | 44 | 36 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.45% | 0.76% | 1.57% | 2.17% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 3.88% | 4.75% | 11.79% | 13.83% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 54.81% | 52.56% | 53.19% | 55.74% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.80% | 4.04% | 9.02% | 12.19% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
### KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA, 2020
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-20 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 6,518 | 5,476 | 18,462 | 17,579 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 4,895 | 5,817 | 16,241 | 13,117 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (24,281) | (167,415) | (206,905) | (170) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (7,686) | 258,871 | 265,134 | 15,984 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 20,268 | 49,893 | 76,313 | (5,632) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 19,742 | (40,933) | (30,757) | (2,084) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (1,700) | (1,774) | (5,249) | (5,175) |
| | - Mengineyo (bainisha) | 33,939 | (100,875) | (77,032) | (37,984) |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | 51,694 | 9,060 | 56,208 | (4,365) |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,459) | (295) | (2,568) | (2,947) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | (1,459) | (295) | (2,568) | (2,947) |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | 12,000 |
| | Mengineyo (bainisha) | (1,148) | (1,908) | (4,553) | 670 |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | *(1,148)* | *(1,908)* | *(4,553)* | *12,670* |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 49,087 | 6,857 | 49,087 | 5,357 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **23,959** | **17,102** | **23,959** | **17,949** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 73,046 | 23,959 | 73,046 | 23,306 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2020
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **60,601** | - | - | **10,220** | **98,893** |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | - | - | - | **13,214** | **13,214** |
| Mapato mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato yaliyohifadhiwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | **14,512** | - | **14,512** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | - | **60,601** | - | **14,512** | **23,434** | **126,619** |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **40,539** | **135** | **3,913** | **10,262** | **82,920** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | 4,048 | **(135)** | **(3,913)** | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 15,891 | - | - | - | **15,891** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hisa za ziada | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (1,210) | - | - | - | **(1,210)** |
| Hasara ya sasa ya manufaa yaliyofafanuliwa | - | - | 133 | - | - | - | **133** |
| Kurudishiwa Gawio lililosimamishwa | | | 1,200 | | | | **1,200** |
| Mengeineyo | | | | | | (42) | **(42)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | - | **60,601** | **0** | **(0)** | **10,220** | **98,893** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA, 2020**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| **SABASABA K. MOSHINGI** (Ofisa Mtendaji Mkuu) | IMESAINIWA | **21.10.2020** |
| **REGINA E. SEMAKAFU** (Mkuu wa Fedha) | IMESAINIWA | **21.10.2020** |
| **SOSTHENES F. NYENYEMBE** (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | IMESAINIWA | **21.10.2020** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA** Mwenyekiti wa Bodi | IMESAINIWA | **21.10.2020** |
| **MR MACRICE D. MBODO** Mjumbe wa Bodi | IMESAINIWA | **21.10.2020** |

Head Office: LAPF Towers Bagamoyo Roard. P.O. Box 9300 Dar es Salaam Tanzania. Telephone: +255 22 2162940, Fax: +255 22 2114815, Email: info@tpbbank.co.tz

## TANGAZO

# TPB BANK MINIMUM DISCLOSURE OF RATES AND CHARGES

| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES |
|---|---|---|
| Minimum Opening Balance | Quick Account | 20,000 |
| | Salary Account | FREE |
| | Platinum Account | 15,000 |
| | Call Account | 100,000 |
| | Minor Account | 20,000 |
| | Scout Minor | 10,000 |
| | Scout | 30,000 |
| | WADU | 20,000 |
| | YANGA VIP Card | 1,200,000 |
| | YANGA Member Card | 25,000 |
| | Group Account | FREE |
| Bank Statement | | Within a month it is FREE and more than a month is 1500 per document |
| Monthly Maintenance Fee | Savings Account | 1,560 |
| | Platinum Account | 1,560 |
| | WADU Account | FREE |
| | Call Account | 6,500 |
| | Minor Account | FREE |
| | Group Account | FREE |
| Dormant Accounts Fee | 1 year to 5 years | 1,300 |
| | 6 years to 10 years | 5,000 |
| | 11 years to 15 years | 10,000 |
| Activation of Dormant Account | | FREE |
| ATM Charges | ATM Balance Enquiry- All cards | 300 |
| | Mini statement | 300 |
| | Cash Withdraw on TPB ATMs | 1,300 |
| | Cash Withdraw on other UMOJA SWITCH ATM | 1,300 |
| POS Branches | Balance Enquiry | 150 |
| | Mini statement | 150 |
| | Deposit | FREE |
| | Transfer | 650 |
| | POS Withdraw | 2,600 |
| POS Agents | Balance Enquiry | 100 |
| | Mini statement | 200 |
| | Deposit | FREE |
| | Transfer | 650 |
| | POS Withdraw | see Tiered Fees 1 |
| Mobile Banking | Balance Enquiry | 300 |
| | Mini statement | 300 |
| | Full Statement | 400 |
| | Pin Charge | FREE |
| | Notification /Alert | 250 |
| | Account Transfer | FREE |
| | Mobile Agent Deposit | 200 |
| | Mobile Agent Withdraw | see Tiered Fees 2 |
| | Mobile Money to Bank Deposit | 1,300 |
| Closing Account | | 13,000 |
| FDR Min. Opening Balance | | 100,000 |
| ATM Issuance and Replacement Fees | Popote Card | 15,000 |
| | Yanga Member card | 20,000 |

| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES |
|---|---|---|
| Other ATM & Normal Card | Pin Re-issue | FREE |
| | Collection of ATM crad at Non Domicile Branch | 6,500 |
| | Uncollected and destroyed ATM card | 6,500 |
| | First ID card (Local and Foreign Currency) | 4,000 |
| | Replacement Of ID card | 2,600 |
| Cash withdraw | Teller withdraw upto 10,000,000 | 2,600 |
| | Teller withdraw from 10,000,001 to 50,000,000 | 5,000 |
| | Teller withdraw from 50,000,0001 to 100,000,00 | 15,000 |
| | Teller withdraw above 100,000,001 | 30,000 |
| Cheques Fees | Cheques Clearing Fee | 3,000 |
| | Special Clearance | 50,000 |
| | Dishonoured Cheque | 35,000 |
| Electronic Fund Transfer (EFT) | TISS Inwards | FREE |
| | TISS- Outward | 10,000 |
| Standing Order | Within the Bank | 1,300 |
| | To other Banks | 13,000 |
| POS Withdraw &Money Transfer/ Tiered fees | POS Withdraw | Tiered 1 |
| Tiered 1 | 0-10,000 | 800 |
| | 10,000-20,000 | 1,250 |
| | 20,001-50,000 | 1,500 |
| | 50,001-100,000 | 2,250 |
| | 100,001-200,000 | 2,750 |
| | 200,001-300,000 | 4,200 |
| | 300,001-400,000 | 5,500 |
| | 400,001-500,000 | 6,000 |
| | 500,001-700,000 | 6,500 |
| Tiered 2 | TPB Mobile Transfer Fee | Tiered 1 |
| | 500-10,000 | 850 |
| | 10,001-50,000 | 1,200 |
| | 50,001-100,000 | 1,500 |
| | 100,001-250,000 | 2,800 |
| | 250,001-500,000 | 4,600 |

## RATES AND CHARGES FOR USD ACCOUNT

| | | |
|---|---|---|
| Maintenance Fee | Savings Account | 1 |
| | Call Account | 5 |
| Deposit Fee | Non Account Holder | Free |
| Opening Balance | | 50 |
| Account closure fee | | 10 |
| Bank Statements | | Free |
| | Balance Enquiry- Banking Hall | Free |
| | Confirmation letter | Free |
| Withdraw Fees | Below 50 | 1 |
| | 51-1,000 | 2.5 |
| | 1,001-2,250 | 5 |
| | 2,251-5,000 | 15 |
| | Above 5,000 | 0.25% |
| Cheque | Any amount | 1.3 USD (TZS Equivalent) |
| | Special Clearance | 40 |
| | Unpaid cheque-Refer to Drawer | 10 |
| | Special Payment | 20 |
| Dormant | Dormant Account Fee | 5 |
| | Re- Activation | Free |
| TISS | | 10 |

Tpb Bank Grow with us

+255 787 669 977 tpbbank//facebook tpbbank//instagram www.tpbbank.co.tz

## LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES

### 1. FEES ON CONSUMER LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 1. | Consumer Loan Administration Fee | 1.5% of the Approved Loan. |

### 2. FEES ON WASTAAFU LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 2. | Loan Application Fee | TZS. 10,000/= |
| 3. | Loan Administration Fee | 1.5% Minimum. TZS. 10,000/= Maximum TZS. 100,000/= |

### 3. OTHER CHARGES ON INDIVIDUAL MICRO CREDIT

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 1. | MIC Loan Application Fee | TZS. 20,000/= |
| 2. | MIC Loan Processing/Administration Fee | 1.5% Minimum TZS. 50,000/= |

### 4. INTEREST RATES AND OTHER CHARGES ON BUSINESS LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 1. | Loan Application Fees for Business and Personal Loans | TZS. 50,000/= |
| 2. | Loan Administration Fee - Business and Personal loans | 1.5% of the Approved Amount |



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# NEC, vyama vya siasa waridhiane mawakala

**SUALA** la kuwaapisha mawakala wa vyama vya siasa limekuwa gumzo hasa kutokana na utaratibu wa kuwataka kusafiri hadi Ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya ambaye ni msimamizi wa uchaguzi wa majimbo wilayani kwake, kula kiapo.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), hivi karibuni ilitoa maagizo hayo utaratibu wa kula kiapo na kazi ya kuwaapisha mawakala ilianza mapema wiki hii.

Viongozi wa baadhi ya vyama vya siasa na mawakala hao wameonyesha kutoridhika na utaratibu huo, wakieleza kasoro nyingi.

Mojawapo ni madai ya kutopewa nakala za viapo, kuahirisha kuwaapisha wakati wengine wametembea umbali mrefu na kukosoa kuwa si utaratibu wa kisheria na masuala ya uwezekano wa wengi kukosa nauli kufika ofisi za wakurugenzi.

Kimsingi tunaamini kuwa NEC ina malengo mazuri ya kutimiza majukumu ya kusimamia uchaguzi na kudhibiti mienendo ambayo inaweza kutatiza mchakato huo wa kidemokrasia.

Kwa mantiki hiyo tunashauri NEC na viongozi wa vyama vya siasa walitafutie ufumbuzi suala hilo, wasimamie na kuwaapisha mawakala wa uchaguzi kwa njia inayokubalika na kuondoa uwezekano wa kusababisha mambo yanayowaumiza watu.

Mathalani, kuna Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2004 ambayo inaelezea namna ya kuwaapisha mawakala hao, NEC iangalie utaratibu rafiki unaowezesha mchakato huo kufanyika kwa amani.

Tunafahamu kuwa kuna maelekezo ya kikatiba yanayoipa NEC mamlaka ya kutimiza wajibu wake bila kuingiliwa au kusikiliza chochote kutoka kwa yeyote, hayo ni mambo yanayotajwa kwenye ibara ya 74 ya Katiba, kifungu cha 11 na 12 kinachoipa NEC mamlaka ya kufanya inavyotaka.

Pengine haya ni miongoni mwa mambo ambayo yanatakiwa kurekebishwa ndani ya katiba ili kuifanya Tume hiyo kuwa ya kidemokrasia na inayowajibika kwa Watanzania.

Kifungu cha 11 cha Katiba kinasema katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi ya Taifa haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya serikali, au maoni ya chama chochote cha siasa.

Aidha kifungu cha 12, kinasema hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote lililotendwa na Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.


Ikumbukwe kuwa uchaguzi ni mchakato unaoshirikisha wadau wengi na jambo muhimu kwa nchi yetu ni lazima liende kwenye utaratibu wa kusikilizana na unaokubalika na wengi.

Tukumbuke, wadau wa uchaguzi ni wengi kuna vyama vya siasa, wagombea, wapigakura, NEC, wasimamizi majimboni ambao ni wakurugenzi wanaowaapisha mawakala, kuna waangalizi wa kitaifa na kimataifa pamoja na wadau wengine wa kimataifa ukiwamo Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika.

Ndiyo maana tunasema cha msingi ni maridhiano na kufanikisha mchakato huo kwa amani. Tunajua Katiba, Bunge na Baraza la Wawakilishi ndivyo vilivyohusika na mchakato wote wa kisheria na taratibu za uchaguzi, lakini sheria na kanuni si misahafu kuwa haiguswi, tunashauri kuwa na hekima, maridhiano na uvumilivu wa kisiasa katika kufanikisha uchaguzi huu, linapokuja suala la kuapisha mawakala.

Ni vyema Katiba, sheria na taratibu za uchaguzi zikatumika kusimamia mchakato huo, lakini na hekima nayo ipewe nafasi yake ili kuongoza na kufikia hatima inayomfurahisha na kumridhisha kila aliyeshiriki kupata viongozi kupitia mchakato wa kupiga kura.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Uchaguzi ndio huo, amani iko mikononi mwetu sote



Na Beatrice Moses, TUDARCO

**NISEME** Jumatano ijayo ndio siku iliyotarajiwa katika kila namna, kwa ajili ya Watanzania kupata viongozi, marais wa Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, pia wabunge, madiwani na mashehia kwa Zanzibar.

Ni uchaguzi mkuu ambao serikali hizo imeitenga kuwa ni maalum, kila mwananchi mwenye sifa anapaswa kuitumia kwenda kupiga kura kuchagua viongozi hao.

Inajulikana kila mwananchi aliye makini na alipata nafasi nzuri ya kufuatilia kampeni za vyama vya siasa vinavyoshiriki kwenye uchaguzi huu, ambao wagombea wa nafasi husika walipata nafasi ya kunadi ilani za vyama vyao. Imempa nafasi nzuri kusikiliza na siku hiyo ataitumia kumchagua aliyemshawishi kwa sera husika.

Mchakato wa uchaguzi katika hatua za kampeni tumeshuhudia mengi, ikiwamo baadhi ya wanasiasa kudaiwa kutumia isivyo majukwaa ya kampeni, kiasi cha kusababisha Tume ya Uchaguzi (NEC), kutoa adhabu kulingana na kanuni walizojiwekea ambazo zipo wazi.

Sasa imefika hatua inayoenda katika kipindi cha lala salama ambayo inatakiwa iwe kweli na usalama kwa nchi na wananchi kwa ujumla, ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anazingatia mwongozo uliotolewa na NEC wakati wa kupiga kura na kusubiri matokeo. NEC katika mwongozo wake, inabainisha mambo kadhaa yaliyogawanywa katika makundi maalum kulingana na makundi ya watu husika, ikiwamo watu wanaoruhusiwa kuwapo katika Kituo cha Kupigia Kura.

Inaelezwa, utangazaji matokeo ya madiwani katika kila kata, matokeo ya wabunge hufanywa na wasimamizi wa uchaguzi na urais ambayo hutangazwa. Mwongozo huo unabainisha watu wanaoruhusiwa kuwamo katika kituo cha kupigia Kura kuwa ni pamoja na Msimamizi wa Uchaguzi na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Wasimamizi wa Uchaguzi.

Hapo ni kwamba, wapo wanaowajibika kwa Mkurugenzi wa NEC na husaidiwa na Wasimamizi Wasaidizi wa uchaguzi.

Katika mwongonzo huo, inabainishwa kwamba wasimamizi wa shughuli zao kituoni, hapo ni kuratibu na kuendesha uchaguzi katika majimbo na kushughulikia na masuala yanayohusu wafanyakazi, uteuzi vifaa, mipango ya upigaji kura, mafunzo na kuhesabu kura.

Mengine yanatajwa kuwa ni kujumlisha na kutangaza matokeo ya madiwani na wabunge katika kata na majimbo, kuhesabu na kujumlisha matokeo ya uchaguzi wa Rais na kuyatuma kwa Tume ya Uchaguzi.

Inadokezwa, majukumu ya Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura ni kusimamia uchaguzi katika ngazi ya kituo cha kupigia kura kulingana na taratibu za uchaguzi, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha matayarisho ya upigaji kura na vifaa vya kupigia kura yamekamilika.

Hiyo inaendana na kusimamia mchakato wa kupiga kura pamoja na wasimamizi wa kituo cha kupigia kura na walinzi wa kituo (wakiwamo askari polisi), kusimamia usalama wa kituo, kutoa taarifa kwa msimamizi wa uchaguzi na penye tatizo litakalojitokeza kukifanyika matayarisho, kuhesabu na kutayarisha fomu za matokeo, kutangaza matokeo ya awali.

Msimamizi wa kituo ana jukumu la kuwasilisha matokeo na vifaa vya kupigia kura kwa Msimamizi wa Uchaguzi katika Kituo cha Majumuisho cha Kata.

Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura, husaidiwa kutekeleza majukumu yake na wasaidizi wa vituo na makarani waongozaji, hata hivyo Msimamizi Kituo ndiye mwenye uamuzi katika kituo hicho cha kupigia kura. NEC katika mwongozo wake, inataja wagombea wa udiwani na ubunge, nao wataruhusiwa kuwepo ndani ya vituo vya kupigia kura, kwa mujibu wa sheria na kanuni kwenye kata au majimbo yao husika.

Wengine ni wakala wa upigaji na kuhesabu kura inabainishwa kuwa, hao nao wanateuliwa na vyama vya siasa au wagombea, ili kulinda maslahi ya mgombea katika vituo vya kupigia kura na kituo cha majumuisho ya kura.

Siku saba kabla ya uchaguzi, wakala hao huapishwa na Tume majina yao hutumwa kwa msimamizi wa kituo husika cha kupigia kura, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za taarifa zao.

Majukumu ya wakala yamebainishwa na NEC ni kuangalia kama kuna udanganyifu, kuweka kumbukumbu za masuala yanayojitokeza kituoni kwa kushirikiana na msimamizi au wasimamizi na wasaidizi wao wa kituo, kuhakikisha sheria na taratibu za upigaji kura zinafuatwa. Hayo ni miongoni mwa yanayotajwa wenye mwongozo huo uliotolewa na NEC. Hivyo, ni vizuri wahusika mliopewa dhamana katika uchaguzi huo kuzingatia, ili kuhakikisha utulivu na amani vinatawala katika vituo vya kupigia kura na uchaguzi unakwisha vizuri.

Wenye dhamira ya kusababisha chokochoko kwenye eneo la uchaguzi tunamuomba Mwenyezi Mungu aliyeshughulikia virusi vya ugonjwa wa maradhi ya Korona, awashughulikie nao wasifanikiwe kuvuruga amani ya nchi yetu kwa sababu ya maslahi binafsi.

## HABARI KITAIFA

# DCB yatoa gawio mil. 287 kwa wanahisa

**Na Romana Mallya**

BENKI ya Biashara ya Dar es Salaam (DCB), imetoa Sh. milioni 287 kwa wanahisa wake wakubwa watatu ikiwamo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam iliyopewa Sh. milioni 138.

Wengine waliopata gawio hilo ni Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja (UTT-Asset Management and Investor Services- UTT-AMIS) Sh. milioni 119 na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Sh. milioni 30.8.

Akizungumza kwenye hafla ya utoaji gawio hilo juzi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Selemani Jafo, alipongeza uongozi wa benki hiyo kwa kuwa mahiri na wenye tija kwa kufanikisha utoaji wa gawio kwa wanahisa wake.

"Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa mafanikio makubwa mliyoyapata kwa kipindi cha miaka 18 tangu kuanzishwa kwa benki hii.

"Natambua kuwa benki hii imeanzishwa kwa malengo ya kusaidia wajasiriamali wadogo na wananchi wa kawaida ili wajikwamue kutoka kwenye umasikini."

Alisema benki hiyo imeweza kujiendesha kwa faida kwa takribani miaka 12 na kutoa gawio kwa wanahisa wake kwa miaka 10 mfululizo, kiasi kinachofikia Sh. bilioni 12.

Jafo alisema alitambua juhudi za bodi ya wakurugenzi na uongozi wa benki za kuhakikisha DCB inapata mtaji kupitia uuzwaji hisa uliokamilika kwa mafanikio mwaka jana.

Waziri huyo alisema serikali inapongeza jumuiya ya benki kupitia Chanma cha Benki Tanzania (TBA) na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa usimamizi thabiti na ushauri ambapo kwa pamoja imesaidia kuendelea kutoa huduma na kuvuka salama katika tatizo la corona.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Godfrey Ndalahwa, alisema fedha zilizotolewa ni sehemu ya gawio la jumla la Sh. milioni 500 ambazo benki italipa wawekezaji wake.

Alisema fedha hizo ni makubaliano yaliyofikiwa katika mkutano mkuu wa 18 wa mwaka wa wanahisa uliofanyika Juni, mwaka huu, kwa njia ya mtandao.

Ndalahwa alisema hiyo ni safari ya kimkakati iliyoanza mwaka 2018 ya kuhakikisha benki inarudi kwenye kupata faida na kujiimarisha ndani ya mwaka mmoja.

"Benki imefanikiwa kuongeza mtaji kupitia uuzwaji wa hisa mwaka 2019 na kuendelea kujiimarisha zaidi, tupo imara kimtaji, kupungua mikopo chechefu, kuongezeka kwa ukwasi na uendeshaji bora huku ikifuata taratibu na miongozo ya usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Mamlaka nyingine za usimamizi za serikali," alisema.

# Wenye kigugumizi watoa tamko

**Na Christina Mwakangale**

JAMII ya watu wenye kigugumizi nchini, wameitaka jamii kuondokana na dhana kwamba walio na tatizo hilo wana matatizo ya afya ya akili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Mitindo Maalum ya Uzungumzaji Tanzania (CHAMMUTA), Ally Abdallah, alisema hayo jana katika maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Kigugumizi Duniani yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, huku akibainisha kuwa kigugumizi si ugonjwa.

Abdallah alisema kutokana na wanaozungumza kwa kigugumizi kuchukua muda wa sekunde kadhaa kuwasilisha ujumbe, hupata matatizo na mazingira magumu kwa kuwa jamii baadhi ya watu hawana subira katika kusilikiza.

"Kigugumizi si ugonjwa, wapo wanaosema watu huzaliwa hivyo hususan wakati wa utoto.

"Dunia inakwenda kasi, watu wenye kigugumizi tuna mazingira magumu sana, unazungumza na mtu ambaye hana subira. Hawataki kutuacha tumalize kuzungumza, wanatukatisha," alisema Abdallah.

Alisema binafsi alikumbwa na tatizo hilo baada ya kufiwa na baba yake, akiwa na umri wa miaka mitano.

"Nilipata msiba wa baba yangu, baada ya miezi michache nilipata kigugumizi kwa mujibu wa mama. Nilipata mshtuko," alisema mwenyekiti huyo.

Alifafanua kuwa baadhi ya watu wanaodhani kwamba mwenye kigugumizi ana ukosefu wa akili, ni dhana potofu inayofanya kundi la watu hao kuhisi kunyanyapaliwa.

"Kigugumizi hutokea na wengine husema mtoto anaweza kumwona mtu mwenye kigugumizi naye akamwiga, vyote vipo kwenye utafiti hakuna uhakika kama vina ukweli," alisema na kuongeza:

"Usimkatishe mwenye kigugumizi anapozungumza, anammaliza kabisa, msubirie hadi amalize sentensi yake."

Mwanasaikolojia Salahudeen Kimangale alisema kigugumizi hakina sababu moja na mtu anaweza kupata kibaiolojia, kijamii na kisaikolojia.


BIASHARA ZOTE MAKINI
HUTANGAZWA HAPA
Nipashe Nipashe mwendo mdundo
Unafahamu ni kwa nini?
"Tunaongoza na Kuaminika"




Nipashe MWANGA WA JAMII
WASILIANA NASI
0745 700 710 au 0677 020 701
advertise@guardian.co.tz (Matangazo)
subscription@guardian.co.tz (Magazeti)
epaper@guardian.co.tz (epaper)
PATA NAKALA YAKO
https://epaper.ippmedia.com
Pakua The Guardian-IPP Media
App Store Google Play
KUWA WA KWANZA KUHABARIKA
TUFUATE nipashetz nipashe TheGuardiantz YouTube TheGuardiantz

# TANGAZO

BancABC part of atlasmara

## AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBER 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Sep-20 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 2,660 | 3,427 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 8,491 | 5,683 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 35,054 | 33,857 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,509 | 4,390 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 187 | (58) |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 103,136 | 100,334 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 138,410 | 127,070 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 31,131 | 32,616 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 3,376 | 3,480 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **324,953** | **311,799** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 106,974 | 100,654 |
| 18 | Amana za Wateja | 100,074 | 93,439 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | 28 |
| 27 | Dhima Nyingine | 2,349 | 2,737 |
| 28 | Madeni | 73,533 | 72,301 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **282,930** | **269,159** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **42,024** | **42,640** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 122,954 | 122,954 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 1,065 | 1,065 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (81,099) | (81,099) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (1,600) | (983) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 704 | 704 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **42,024** | **42,640** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 4,175 | 3,207 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 24,142 | 24,477 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 17,163 | 17,171 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 12.93% | 13.68% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 15.59% | 17.05% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 75.14% | 74.32% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 42.59% | 40.75% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 85.58% | 85.20% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 6.67% | -1.84% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 4.22% | -1.93% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBER 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-20 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 11,191 | 10,859 | 32,078 | 32,045 |
| 2 | Gharama za Riba | (5,113) | (4,699) | (14,542) | (14,152) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **6,078** | **6,160** | **17,537** | **17,894** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 439 | 566 | 1,294 | 1,663 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | (700) | (520) | (2,154) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **940** | **1,380** | **2,856** | **3,997** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 349 | 434 | 1,052 | 1,432 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 400 | 814 | 750 | 2,191 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 191 | 132 | 1,054 | 374 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(8,040)** | **(8,704)** | **(22,665)** | **(24,695)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,567) | (2,750) | (7,588) | (8,077) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (5,473) | (5,953) | (15,077) | (16,618) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(583)** | **(1,297)** | **(1,498)** | **(3,297)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (34) | - | - | - |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(617)** | **(1,342)** | **(1,600)** | **(3,433)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(617)** | **(1,342)** | **(1,600)** | **(3,433)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 153 | 156 | 153 | 156 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.00) | (0.55) | (0.00) | (0) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 7 | 6 | 7 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.26% | -1.71% | -0.67% | -1.45% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -1.94% | -10.23% | -5.04% | -8.72% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 114.56% | 115.43% | 111.14% | 112.81% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.19% | 3.64% | 3.44% | 3.53% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBER 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-20 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (583) | (316) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | (202) | 1,426 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (10,849) | (191) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | (10) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 12,955 | (3,773) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (1,197) | (524) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 816 | (3,236) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 1,485 | (226) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (34) | (34) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **2,390** | **(6,883)** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (184) | (88) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(184)** | **(88)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 2,206 | (6,971) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 113,776 | 120,747 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **115,982** | **113,776** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBER 2020

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(80,525)** | **130** | **0** | **1,065** | **43,624** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (1,600) | - | - | - | (1,600) |
| Hisa za upendeleo | - | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (574) | 574 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(82,699)** | **704** | **0** | **1,065** | **42,024** |
| | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **116,014** | **-** | **(72,910)** | **0.22** | **1,284** | **1,065** | **45,453** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (8,769) | - | - | - | (8,769) |
| Hisa za upendeleo | 6,940 | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (130) | 130 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 1,284 | - | (1,284) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(80,525)** | **130** | **0** | **1,065** | **43,624** |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 23-Oct-20 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 23-Oct-20 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 23-Oct-20 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| **1** Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 23-Oct-20 |
| **2** Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 23-Oct-20 |

# CWT yatoa likizo siku 5 walimu kushiriki uchaguzi

**Na Elizabeth Zaya**

ZIKIWA zimebaki siku tano kuelekea uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani, Chama cha Walimu Tanzania (CWT), kimetoa siku tano za mapumziko kwa watumishi wake kuanzia Oktoba 26 hadi 30, ili kutoa fursa kwa watumishi hao kushiriki vyema katika uchaguzi huo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyosainiwa na Katibu wa Chama hicho, Deus Seif, watumishi wote wa CWT wanatakiwa kurudi kazini Novemba 2, mwaka huu.

"Oktoba 28, 2020 ni siku ya uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani wa Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni rais, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na madiwani," ilieleza taarifa hiyo. "Ili kutoa fursa kwa watumishi wa CWT kushiriki kupiga kura katika maeneo waliyojiandikisha, ofisi imetoa mapumziko ya siku tano kuanzia 26 hadi 30, Oktoba 2020. Watumishi wote wanatakiwa kuwapo kazini Novemba 2."

Wakati CWT ikitoa likizo kwa watumishi wake, tayari Rais John Magufuli alishatangaza Oktoba 28, kuwa siku ya mapumziko kwa lengo la kutoa fursa kwa kila mwananchi kushiriki katika uchaguzi huo.

Katika mikutano yake tofauti kwenye kampeni zinazoendelea, Rais Magufuli, alisema atatangaza rasmi siku hiyo kuwa ya mapumziko.

## TAKUKURU yawanoa wanahabari kuhusu uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu,** SONGEA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Ruvuma imetoa mafunzo ya kuripoti habari za uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Katika mafunzo hayo ambayo yalifanyika jana kwenye ukumbi wa TAKUKURU Mkoa mjini hapa, mwanasheria wa taasisi hiyo, Herman Malima, alisema waandishi wa habari wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kuwaelimisha wananchi madhara ya kupata viongozi kwa njia ya rushwa.

Sambamba na hilo, alisema wanahabari wanapaswa kuwa mfano wa kuigwa katika mapambano dhidi ya rushwa kwa sababu wao ni kioo cha jamii. Alisisitiza kwa waandishi wa habari wasiandike taarifa ambazo zinaweza kusababisha uchochezi kwa wanasiasa na jamii kwa sababu kwa kufanya hivyo, wanaweza kuleta machafuko na ukosefu wa amani katika taifa.

"Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985 inahusika na kuongoza uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani na inatoa taratibu za uchaguzi na mamlaka mbalimbali ikiwamo kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC). Sheria hii inakemea vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi na inaelekeza adhabu," alisema Malima.

Mwanasheria huyo alionya viongozi wanaochaguliwa kwa njia ya rushwa hawafai kwa sababu wanaweza kusababisha kudumaza uchumi kwa kuwa watakuwa viongozi wasiopambana na rushwa kwa ukamilifu.

Akizungumza wakati anafungua mafunzo hayo, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma, Hamza Mwenda, aliwataka wanahabari kuhakikisha wanaripoti habari za uchaguzi kwa weledi na maadili ili kutosababisha machafuko.

Alisema mafunzo hayo yataongeza umakini na uangalifu katika kutafuta, kuchuja na kusambaza habari mbalimbali zitakazokuwa zinaandikwa katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu.

# Mwambe kudai Masasi iwe mkoa

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

MGOMBEA ubunge Jimbo la Masasi mjini kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Geofrey Mwambe, amemwomba Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, iwapo chama hicho kikiingia madarakani, serikali ihakikishe inaipatia Wilaya ya Masasi mkoa mpya ili kupanua wigo wa fursa za kimaendeleo kwa wananchi wa wilaya hiyo.

Mwambe alitoa ombi hilo jana mbele ya Waziri Mkuu, wakati alipokuwa akimwombea kura Rais Dk. John Magufuli, kwenye mkutano wa hadhara wa kampeni, uliofanyika katika viwanja wa Sabasaba mjini hapa. Alisema Serikali ya Mapinduzi kupitia Ilani yake CCM katika kipindi cha miaka mitano imefanya maendeleo makubwa katika mji wa Masasi ikiwamo kuboresha sekta ya elimu, afya na miundombinu ya barabara.

Mwambe alisema sekta zingine ambazo zimetekelezwa kwa kiwango kikubwa ni barabara, huduma ya maji na afya na yeye kama mgombea pia ataendeleza kupanua huduma hizo.

Alisema moja ya jambo ambalo akipata ridhaa ya kuchaguliwa kuwa mbunge wa Jimbo la Masasi ni kuhakikisha Wilaya ya Masasi inapata kuwa mkoa wake unaojitegemea.

Alisema mchakato huo wa kuomba mkoa ni mwendelezo ambao ataufanya kama mbunge wa jimbo hilo na ni mchakato uliofanyika tangu mwaka 2013/ 2014, lakini ulikwama ghafla. Alisema mji wa Masasi kwa sasa una hadhi kubwa kwa mikoa ya Kusini na una uwezo wa kujitegemea kuwa mkoa, hivyo anaiomba serikali ikiingia madarakani Wilaya ya Masasi iwe mkoa.

"Mheshimiwa Waziri Mkuu Wanamasasi wamesema wanampenda sana Rais Dk. John Magufuli na watamchagua kwa kura nyingi za kishindo na watanichagua mimi kuwa mbunge wao wa Masasi mjini, lakini wananchi hawa wanaomba mkoa wao," alisema Mwambe. Alisema akiwa mbunge wa Jimbo la Masasi atahakikisha huduma zote muhimu anazifanyia kazi ili mji huo uweze kuwa mji bora na wakisasa.

Alisema atahakikisha Hospitali ya Mkomaindo inapandishwa hadhi na kuwa hospitali teule kwa kuwa ina sababu ya kupandishwa kutokana na huduma zinazotolewa. Kadhalika, aliwaomba wananchi wa jimbo hilo kuwa na imani kwake pamoja na wagombea wote wa Chama Cha Mapinduzi wawachaguwe ili waweze kuleta maendeleo chanya kwao.

Waziri Mkuu, Majaliwa alisema jambo hilo analibeba na kuwataka wananchi wa wilaya hiyo kujitokeza kwa wingi Oktoba 28, kuichagua CCM kwa kishindo.


BancABC part of atlasmara

AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | Free | Free | Free |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| CURRENT ACCOUNT | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 2,000.00 | N/A | N/A |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 2,000,000.00 | $ 2,000.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 5,000.00 | $ 10.00 | N/A |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 3,000,000.00 | $ 3,000.00 | £ 3,000.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | £ 1,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | £ 5,000.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NIL | NIL | NIL |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NIL | NIL | NIL |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 120.00 | N/A |
| Technical | TZS 60,000.00 | $ 60.00 | N/A |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 30,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| 100 leaves | TZS 60,000.00 | $ 60.00 | £ 60.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 10% Per Cheque | 10% Per Cheque |
| **Stop Payment Charges** | TZS 60,000.00 | $ 60.00 | £ 50.00 |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | TZS 10,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | TZS 4,000.00 | $ 3.00 | £ 2.00 |
| Standing Order - Other local bank | TZS 40,000.00 | $ 30.00 | £ 20.00 |
| Amendment | TZS 5,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| - Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| - Cash Deposit at Branch small denominations 500 above 50 | 0.3% Min 1,000 | 3% On Small denominations | N/A |
| - Cash Deposit at Branch small denominations (2,000 and be | 0.3% Min 1,000 | 3% On Small denominations | N/A |
| - Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 0.3% Min 1,000 | N/A | N/A |
| With Account Transfers (Internal) | N/A | N/A | N/A |
| - Cheque deposit | Free | Free | Free |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to | TZS 2,500.00 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 5 | TZS 6,000.00 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) abov | 0.15% MAX 200,000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3000 Max 200000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 7,500 Max 200,000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| - Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 2%On small denominations* | 2%On small denominations* |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account monthly fee | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 5,000.00 | $ 3.00 | £ 3.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Reference Letter | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | Comm 0.25% Min 50 Max 500 | comm 0.25% min 50 max 350 |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% per qtr min $200 | 1% per qtr min $200 |

# Pinda ahimiza kuilinda amani

**Na Neema Hussein,**

MPANDA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amewataka Watanzania kutumia nguvu zao kuitunza na kuilinda amani na kuiona ndiyo tunu muhimu kwa taifa.

Pinda alisema hayo jana wakati akiwaombea kura wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kata ya Kakese, Manispaa ya Mpanda.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo amani ipo ya kutosha, hivyo akasisitiza kuendelea kuitunza huku akibainisha kuwa ilani ya uchaguzi ya CCM imeweka wazi kuwa itaendelea kuilinda tunu hiyo.

"Bila amani tukianza kuvurugana hapa hakuna maendeleo. Hakuna atakayelima, hakuna atakayetembea kwa uhuru. Wako watakaopata matatizo makubwa zaidi hasa wazee, watoto, wenye ulemavu na kinamama," alisema.

Pinda alisema ilani hiyo imeahidi pia katika miaka mitano ijayo, endapo mgombea urais wa CCM, Dk. John Magufuli na mgombea ubunge wa Mpanda Mjini, Sebastian Kapufi, watajitahidi kujenga uchumi kupitia viwanda vinavyotumia malighafi kutoka kwa wakulima, wafugaji na wavuvi.

Alisema chama hicho kina sera zinazojali Watanzania na kimejitahidi kuwa na wagombea wazuri na uzoefu wao katika kusimamia ilani ambazo zimeleta maendeleo ya watu.

Kwa upande wake, Kapufi alisema endapo watamchagua ataboresha barabara, elimu, maji, afya na michezo ikiwa ni mwendelezo wa yale aliyoyafanya awamu iliyopita.

Kapufi alimshukuru Rais Magufuli kwa kuifikisha nchi ilipo sasa, hivyo kuwaomba wananchi kumtia moyo kwa mara nyingine kwa kumpigia kura rais huyo.

# Serikali kukatia wananchi wasio na uwezo bima ya afya

**Na Joseph Mwendapole,**
DODOMA

SERIKALI imesema mpango wa bima ya afya kwa wote uko katika hatua nzuri na Watanzania wote ambao hawatakuwa na uwezo wa kukata bima hiyo watakatiwa na serikali.

Hayo yalisemwa jana mkoani hapa na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Edward Mbanga, wakati akifungua mkutano wa siku moja kati ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), wahariri na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari.

Alisema majadiliano kuhusu kuanza kwa mpango huo bado yanaendelea kati ya serikali na wadau, ili kuhakikisha kwamba utakapoanzishwa Watanzania wote wakiwamo wasio na uwezo wanapata huduma hiyo. "Watu wanaweza kujiuliza mbona mpango huu umejadiliwa muda mrefu, lakini serikali makini huwa haikurupuki kufanya mambo yake ndiyo sababu tunataka kuhakikisha hata wale wasio na uwezo kabisa hawaachwi na uzuri ni kwamba mpango huu umefikia katika hatua nzuri sana," alisema.

Alisema pamoja na umuhimu wake kwa afya za watu, bado kuna Watanzania wengi ambao hawajakata bima ya afya jambo ambalo linaweza kuwasababishia kukosa huduma za matibabu watakapougua wakiwa hawana fedha mifukoni mwao.

"Katika Watanzania wote zaidi ya milioni 50 ni watu milioni nne tu ambao wamekata bima ya afya kwenye mfuko wa NHIF hivyo nyinyi waandishi wa habari mna kazi kubwa ya kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa bima ya afya kwa sababu safari bado ni ndefu sana," alisema.

Vilevile, alisema serikali itawachukulia hatua watoa huduma wote wa bima ambao watachelewesha au kukwaza utoaji wa huduma bora za matibabu ili kuwahakikishia Watanzania wote huduma bora za matibabu wanapougua.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema mfuko huo unatarajia kutimiza miaka 20 ya utoaji huduma mwaka 2012 ukijivunia mafanikio lukuki yaliyopatikana kwa kushirikiana na wadau mbalimbali nchini.

Konga alishukuru vyombo vya habari kwa namna ambavyo vimekuwa vikishirikiana na mfuko huo kutoa habari zake hali ambayo imechangia uwe mfuko bora wa bima ya afya.

Alisema kulinganisha na mifuko na taasisi zingine za bima ya afya, NHIF imepata uzoefu mkubwa kwa miaka yote hiyo ya utoaji wa huduma kwani kwa muda wote huo imewahudumia mamilioni ya Watanzania.



Mtaalamu wa maabara katika kliniki ya Moyo ya Heameda, Abdulkarim Abdallah, akiendelea na majukumu yake wakati wa sherehe za maadhimisho ya miaka 10 ya utoaji huduma ya kliniki hiyo, iliyopo Bunju jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jamii yaonywa kufumbia macho ukatili

**Na Yasmine Protace**

JAMII imetakiwa kutoa ushirikiano inapoona kuna matukio ya ukatili ili hatua zichukuliwe dhidi ya wahusika.

Pia imetakiwa kutoyafumbia macho matukio ya ukatili, ikiwamo kumalizana na wahusika na badala yake kutoa ushirikiano ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Nyegulila Mwaseba, katika semina ya Jinsia na Maendeleo ya Jamii (GDSS) inayoratibiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Alisema usiri unafanywa na waliofanyiwa ukatili unachangia hata kutochukuliwa hatua mtu aliyefanyiwa vitendo hivyo.

"Tuwe na umoja, tukiona ukatili umefanyika sehemu yoyote inatakiwa usiri usiwapo ili wahusika wachukuliwe hatua," alisema Mwaseba.

Aliongeza kuwa mahakama ni chombo kilichoundwa kikatiba kwa ajili ya kusimamia utoaji wa haki na kwamba ziko sheria mbalimbali zinazohusika katika uendeshaji wa mashauri ya watu waliofanyiwa ukatili.

Kwa mujibu wa Mwaseba, jukumu kubwa la mahakama ni kusikiliza mashauri mbalimbali na kuyatolea uamuzi.

"Matukio ya ukatili yapo, watoto wanafanyiwa ukatili, lakini familia zinaogopa kusema kutokana na vitisho zinavyovipata kutoka kwa watuhumiwa," alisema.


Aliongeza kuwa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura namba 20 kama ilivyorekebishwa mwaka 2019, inahusika namna ya uendeshaji wa mashauri ya jinai ikiwamo ukatili.

Naibu Msajili huyo alisema sheria hiyo inaeleza iwapo kosa husika lina dhamana au halina na inataka upelelezi ukamilike kwa muda gani.

Alisema vikwazo ambavyo wanakutana navyo katika mashauri ya ukatili ni pamoja na watu kumalizana nje ya mahakama, mashahidi kubadili mawazo, mashahidi kutokufika mahakamani na kutojidhamini mahakamani.

Bishagazi Selemani, mmoja wa wanaharakati na Mkurugenzi wa Kituo cha Maarifa ya Jamii Kipunguni, alisema kuna haja ya kutolewa mafunzo kwa wanajamii.

Selemani ambaye alishiriki katika GDSS, alisema elimu ikitolewa italeta mabadiliko kwa jamii, kutokana na sasa baadhi ya watu kuwa na uelewa mdogo katika kuzijua haki zao.




Ukurasa 13

Jamani amani na iwe kwenu Watanzania

BUFE

IJUMAA OKTOBA 23, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

MAMBO YA JUMATANO IJAYO...

**Petroli waahidi uhakika kona zote itakapofika siku uchaguzi wauza**

UCHUMI

# Wajasiriamali wapatiwa ubunifu mpya, taka majumbani zinapogeuzwa mkaa

**Na Yasmine Protace**

ELIMU ya ujasiriamali inapotolewa sehemu husika mara nyingi inakuwa ni mkombozi katika sehemu hiyo.

Imekuwa ikishuhudiwa kinamama na wanaume wakipatiwa mafunzo ya ujasiriamali katika lengo la kuwainua kiuchumi ndani ya mazingira yao.

Hivi karibuni, wanakikundi cha Sauti ya Jamii, kutoka eneo la Kipunguni, Wilaya ya Ilala nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam, wamepatiwa mafunzo ya kutengeneza mkaa kwa kutumia chenga zake na maboksi.

Lengo la mafunzo hayo, ilikuwa kuwawezesha wainuke kiuchumi kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka mahali walipo, zikiwamo taka ngumu.

Mkurugenzi wa Kituo ha Maarifa ya Jamii, Selemani Bishagazi, anasema mafunzo hayo yanalenga kuwasaidia kinamama hao kujinasua kimaisha na kuinuka kiuchumi, kupitia matumizi ya taka zilizopo, ili kuzigeuza nishati mkaa.

Anasema, mafunzo ya kutengeneza nishati mbadala waliyapata kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na sasa walikuwa wanapeleka mrejesho mahali husika.

"Mafunzo ya kutengeneza Nishati mbadala yakitolewa na TGNP Mtandao, ambapo wanatoa mrejesho kwa jamii," anafafanua mkurugenzi huyo, huku akihimiza waligundua taka zilizopo mitaani zinavyoweza kubadilika fursa kiuchumi.

Bishagazi anasema lengo kubwa lililopo sasa ni kuhakikisha kila kinachopatikana ndani ya mazingira yao chenye sura ya malighafi kinageuzwa fursa kiuchumi, kwani asilimia 60 ya wakazi wa Dar es Salaam, wanatumia mkaa anaoutaja chanzo kikuu ni mkoani Singida.

Katika ushauri wake, anawataka viongozi wakuu kama wabunge ambao sasa wako katika machakato wa kuchaguliwa wiki ijayo, pia mamlaka za halmashauri (kama vile Manispaa ya Ilala), zitoe mafunzo sahihi namna taka zinapaswa kutumika inapogeuzwa kuwa mkaa.

Anafafanua kuna jumla ya vikundi 12 vilivyoaalikwa kushuhudia mkaa utengenezaji mkaa kwa kutumia chenga zake na taka ngumu kutoka mitaani, hali kadhalika majumbani.



Kinamama wakiwa katika maandalizi ya kutengeneza mkaa, baada ya mafunzo: **PICHA ZOTE: YASMINE PROTUS.**



Mkurugenzi wa Kituo Cha Maarifa Kipunguni, Selemani Bishagazi, akiwapa maelekezo kinamama kutoka makundi mbalimbali, jinsi ya kutengeneza mkaa

Mkazi kutoka Pugu Majohe, Flavian John, anakiri elimu hiyo imemsaidia kujua kutengeneza mkaa huo kwa teknokijia na malighafi aina mpya.

Anasema kikundi chao kilikuwa kinajishughulisha na upambaji, lakini baada ya mafunzo hayo ya kuutengeneza mkaa, imekuwa fursa mpya kwao kuhakikisha wanajikwamua kimapato.

Mwingine, Munira Waziri, anasema ameshiriki katika mafunzo hayo, ikiwa ni njia ya kumuwezesha kupata darasa la kisasa kuhusu mbinu ya kutengeneza mkaa kwa kutumia taka zinazomzunguka.

Aziza Juma, anayetokea eneo jirani la Gongo la Mboto Jijini Dar es Salaam, ambako pia si mbali sana na Majohe, ana mtazamo wa sasa kuna mwanga mpya unaoelekea kumbadilishia maisha yake kiuchumi.

" Nilikuwa sijui kama taka zinaweza kutengeneza mkaa. Sasa nimejifunza na nitatumia mafunzo hayo kujiongezea kipato," anasema.

Anafafanua kuwa, katika mtazamo mpana mafunzo hayo yakiendelezwa, yataisaidia jamii kwa ujumla kuanza kupunguza ukataji miti kama chao cha nishati ya moto.

Mwajuma Juma, anasema mafunzo aliyaitisha ili wakusayike na wanavikundi kwa jumla wanufaike kwa pamoja na kuacha kukata miti, kama chanzo cha nishati moto.

Pia, katika hilo anaielezea shukrani asasi ya TGNP Mtandao, kwa kuandaa mafunzo ambayo sasa yamebeba sura ya ukombozi kwa wanadamu hao wahusika

Mama Ester Joseph, anasema kutolewa mafunzo hayo yanafungua mlango wa kutasaidia kupunguza matumizi ya kuni, tendo linaloambatana na ukataji ovyo wa miti.

Ester anaishauri jamii iendelee kuelimishana ili iache kukata miti ovyo na badala yake, umma ujiongeze kifikra na matendo kwa kutumia utengenezaji mkaa kwa mpya, unautokana nan taka ngumu za majumbani.

BIASHARA

# Kupanuliwa bandari kunavyozidi kuwa mtaji wa maendeleo kitaifa na majirani

- Rais Malawi atua, aweka sawa ushirikiano
- Mageuzi makubwa ya bandarini yaja 2024

**Na Mary Geofrey**

MAPEMA mwezi huu, Rais wa Malawi Lazarus Chakwera, aliwasili nchini kwa ziara ya siku tatu, lengo ni kujenga uhusiano baina ya nchini hizi mbili na wanachama wa Umoja wa Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

Malawi inahesima yake nchini, ikiwa imepewa kisheria ardhi ndani ya banadari ya Dar es Salaam, eneo la Bandari linalojulikana kwa jina la Malawi Cargo Centre.

Hilo linatajwa kuwa mwanzo mzuri wa biashara baina ya nchi hiso mbili, kwa sababu Malawi ni nchi isiyo na bandari na inategemea nchi kama Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mizigo yake inayotumia njia ya maji.

Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) ni moja ya taasisi ambazo Rais wa Malawi, alitembelea kiowa nchini kwa ajili ya kufahamu namna inayosaidia kukuza uchumi wa Taifa hili.

Rais Dk. John Magufuli, alimpokea mgeni wake na kufanya mazungumzo kadhaa kabla ya kutembelea Bandari Kuu ya Dar es Salaam, ambayo kama ulivyo usemi unaotangzwa kila mara 'ni lango kuu la uchumi.'

BANDARINI DAR

Rais Chakwera alipokuwa katika Bandari Kuu ya Dar es Salaam, alipokelewa na Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Deusdedit Kakoko, anayemuelezea jukumu lao kuu ni kusimamia, kuendeleza na kusimamia bandari zote za Tanzania zilizopo kwenye mwambao wa Bandari Hindi na maziwa Nyasa, Tanganyika na Victoria.

Anasema bandari ya Dar es Salaam, ndio pekee kuhudumia nchi jirani za Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Rwanda, Uganda, Zimbabwe, Sudani pamoja na visiwa vya Comoro.

"Soko la Malawi ni miongoni mwa masoko yanayokuwa kwa kasi nje ya Tanzania ambalo mzigo wake umefika Tani milioni 1.12 kwa mwaka zinazohudumiwa na bandari za nchi mbalimbali," anasema.

Kakoko anafafanua kuwa zaidi kwamba, katika mwaka 2019/20, kuna jumla ya tani 376,054 zilipita hapo zikiwa mizigo wenye asili ya maji za Malawi, mbolea na magari zilipitishwa mahali hapo.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari, Mhandisi Deusdedit Kakoko, akitoa maelezo kwa Rais Dk. John Magufuli, alipofanya ziara.

Anasema kwamba, takwimu zinaonyesha kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita, kuanzia mwaka 2010/10 mpaka msimu uliopita wa 2019/20, mzigo wa Malawi unaopita katika bandari ya Dar es Salaam, umeendelea na unaongezeka kwa kasi, hali inayoashiria wadau hao wa kibiashara wanaridhika na huduma wanazozipata bandari.

Huku akisema huduma hizo zinaendelea kuboreshwa kila mwaka, mbali na Dar es Salaam, nyingine zinazoboreshwa kunufausha Malawi ni bandari kubwa Mtwara iliyopo Kusini mwa Tanzania.

"Shehena kutoka Bandari ya Mtwara inaweza kusafirishwa kwa njia ya barabara hadi mkoani Ruvuma, kisha kusafirishwa kwa njia ya maji kupitia bandari za Mbamba Bay, Chipata, Nkatha Bay na kuingia nchini Malawi.



Rais wa Malawi akizungumza na wafanyakazi wa Bandari Dar es Salaam (hawapo pichani) alipowatembelea hivi karibuni, alipokuwa nchini.

Anasema, kwa sasa bandari ya Mtwara inatekeleza mradi wa ujenzi wa Gati Namba Mbili, ambayo hadi kukamilika kwake utaongeza uwezo wake wa kuhudumia shehena kutoka Tani 400,000 za sasa, hadi tani milioni 1.5.

Kakoko anasema, nchi ya Malawi inaweza kuhudumiwa na Bandari ya Ziwa Nyasa, ambayo ni ya tatu kwa ukubwa ziwani, baada ya maziwa ya Tanganyika na Victoria.

Anasema, katika Ziwa Nyasa iliyopo upande wa Tanzania, wana bandari kadhaa akizitaja kuwa ni: Mbambabay, Itungi, Kiwira, Matema, Liuli, Ndumbi na Manda.

"Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, mzigo uliosafirishwa kupitia Bandari za Ziwa Nyasa umekuwa ukiongezeka kutoka Tani 3,469 kwa mwaka 2015/16 hadi kufikia tani 11,220 kwa mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia 34.

Mkuu huyo wa bandari, anaendelea kufafanua kwamba katika kuhakikisha bandari za Tanzania zinaendelea kutoa huduma bora kwa wateja wake, serikali nchini imeamua kuziboresha kwa kuzijengea uwezo wa kuhudumia meli na shehena kubwa zaidi.

"Kwa mfano Bandari ya Dar es Salaam, inatekeleza mradi mkubwa wa kuiboresha unaojulikana kama Maritime Gateway Project (DMGP) ambao upo katika hatua nzuri ambao ujenzi wa Gati Namba Moja, Mbili, Tatu na Nne umekamila kwa asilimia 100.

"Ujenzi wa gati la meli za magari (Roro Berth) umefika asilimia 94 na ujenzi huu unatarajiwa kukamilika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/2021," anaeleza Kakoko.

Anafafanua kwamba, TPA ipo katika hatua za mwisho za ununuzi wa kupata makandarasi wanaofanya kazi ya kupanua na kuchimba lango la kuingilia na eneo la kugeuzia meli, kazi inayotarajiwa kuanza wakati wowote katika mwaka wa fedha uliopo wa 2020/21.

Kakoko anasema, mradi wa DMGP utakapomilika mwezi Juni mwaka 2024, Bandari ya Dar es Salaam itakuwa na uwezo wa kuhudumia mzigo wa shehena tani milioni 25 kutoka tani milioni 16 za sasa kwa mwaka .

"Pia Bandari ya Dar es Salaam, itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli zenye urefu wa mita 3030 na zenye uwezo wa kubeba makasha 'TEUS' 8,000 kulingana na meli zenye urefu wa mita 243 zenye kubeba makasha 'TEUS' 4,000 kwa sasa," anasema Kakoko.


JPM AIHAKIKISHIA MALAWI

Kuhusu ujio wa Rais Chakwera, Rais Dk. Magufuli anaahidi kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na Malawi, hususani ndani ya sekta za bandari, kilimo na umeme na Malawi itapewa mbinu za ukusanyaji mapato.

Pia, Dk. Magufuli anawaahidi wananchi wa Malawi, kwamba bandari za Mtwara na Dar es Salaam, itatumika kikamilifu kwa ajili ya kusaidia uchumi wao, huku ikitajwa ni ziara hiyo inayoleta mapinduzi na mafanikio makubwa, wananchi wa Malawi wakiahidiwa kujisikia kuwa na uhuru wa nyumbani, wanapokuja Tanzania.

Ujio wa Rais wa Malawi nchini, ni mwendelezo wa ushirikiano wa Rais Magufuli na marais wa nchi jirani, wanaoendelea kufika nchini kuimarisha uhusiano, hasa wa kiuchumi.


Itakumbukwa Septemba 13, mwaka huu, Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, aliwasili nchini kufanya mazungumzo na Rais Dk. Magufuli wilayani Chato, mkoani Geita, pia Septemba 19, mwaka huu mkoani Kigoma, Rais wa Burundi, Evarist Ndayishimiye, alifika huko.



Sehemu ya Bandari ya Dar es Salaam, **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Jamani amani na iwe kwenu Watanzania






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

MAMA mmoja alikuwa akiishi na bintiye mdogo, wawili tu wakipendana hapana mfanowe. Lakini, katika vitu vya ndani alivyovipenda huyo mama ni chupa yake ya chai, ambayo mara nyingi alihifadhi uji kwa ajili ya bintiye.

Aliipenda chupa hiyo, kwani ni zawadi aliyoletewa na marehemu mumewe kutoka ng'ambo, hivyo hakuwa tayari kuipoteza, kwanza kwa sababu ilimkumbusha mumewe, pia ilihifadhi mlo wa bintiye.

Hivyo, muda mwingi aliutumia kuhakikisha chupa hiyo iko salama, kwani kuvunjika kwake kungemkumbusha kifo cha mumewe, pia kungemnyima raha binti yake na hata yeye sasa angelazimika kila mara kuchemsha uji.

Kwa kuwa aliufahamu utundu wa mwanawe huyo, alihakikisha kila mara inakuwa mbali naye, kwani kosa moja lingekuwa goli kwake. Kila alipoiona iko karibu na bintiye, aliharakisha kuiondoa na kuiweka kabatini.

Lakini, hakujua kumbe mwanawe naye aliipenda hivyo hivyo, kwani alijua lilikuwa linahifadhi uhai wake, hivyo alitamani kila mara awe karibu na 'mama' yake huyo.

Kwa utoto ule, kuna nyakati alikuwa akiidondosha na mama kutumia fursa hiyo kumkanya kwa angalau bakora, na nyakati zingine kumfinya au kumlamba vibao, ili ajifunze kwamba mchezo wake ni hatari.

Watoto walivyo wasahaulifu, tabia haikukoma, hivyo aliendelea kuidondosha na mama pia akaendelea kumkanya kwa njia hiyo hiyo. Aliumia kupigwa kila siku, kwa sababu ya chupa ambayo haina kauli.

Siku moja wazo la kitoto likamjia, kwamba hivi kumbe bila chupa ile, mateso yake yasingekuwapo, hivyo ni bora isiwepo naye apumzike mateso, ingawa siku ya kutoweka kwa 'mama' yake huyo, mateso yangekuwa makubwa.

Akajisemea kuwa ni bora aidondoshe na tena safari hii kwa nguvu ivunike na isiwepo kabisa pale nyumbani na mateso yatoweke. Na kweli siku ya siku mama hayupo, akaibamiza ukutani ikasambaratika.

Potelea mbali liwalo na liwe, bora leo abamizwe yaishe sambamba na chupa ile, ili kesho na keshokutwa kusiwapo tena matatizo ya kufokeana na kuadhibiana kwa sababu tu ya chupa.

Hatimaye, mama aliporejea kutoka alikokuwa, hakika hakuamini macho yake, ingawa alimkuta binti yake akijiliza na kuomba radhi kuwa amefanya kwa bahati mbaya ili asamehewe.

Kwa kuwa alishajiandaa kwa lolote, alikubali kufokewa akavumilia kupigwa, huku akijua 'jini' limeshatoweka na kesho maisha bila chupa ya chai yatakuwa ya amani na mama atalazimika kutafuta mbadala.

Watanzania tuko kwenye kampeni, tunatafuta Rais, wabunge na madiwani. Wenye vyama vyao wanapita huku na kule kuhanikiza sera na ilani zao za uchaguzi, huku wakiomba kura au 'kula'.

Wagombea wanaongoza misafara nchi nzima mkoa kwa mkoa, wilaya kwa wilaya, majimbo kwa majimbo, kata kwa kata na hata nyumba kwa nyumba, wakisaka kura.

Tunasikia ahadi kedekede, ratiba za mikutano zinafuatwa na kwingine zinakiukwa, taratibu za mikutano zinapangwa na kufuatwa, kwingineko zinakiukwa na kuvurugwa, ili mradi kila mtu anataka apate akitakacho.

Viongozi mbalimbali wa kidini wanasimama majukwaani na kwenye majumba ya ibada kuomba amani na kuhimiza amani, huku wengine wakijisahau na kukampeni wagombea wao.

Tume ya Uchaguzi inafuatilia na kukemea kwenye kasoro, huku Jeshi la Polisi nalo likiwaonya wanaotishia amani na usalama kwa Watanzania. Ili mradi kelele njema zinasikika kutoka kila upande wa nchi.

Nia ni njema. wote wanaopiga kelele wanaitakia mema nchi na watu wake. Asiyeelewa sasa ana lake jambo, hivyo sasa tusifanye kuwa kelele hizo zinanyanyasa au zinatisha na zinawapa kichwa wanaolengwa na matokeo yake, wazione ni kero kwao na kisha wajiambie liwalo na liwe.

Tuwe makini hawa walengwa wasijikute wakituvunjia chupa yetu ya amani tunayoipenda tukakosa pa kuhifadhi amani yetu. Sijui mmenielewa? Bila shaka, tunajenga nyumba moja, fito ziendelee kuthaminiwa. Alamsiki!

BIASHARA

MAMBO YA JUMATANO IJAYO...

# Wauza Petroli nchini waahidi uhakika kona zote itakapofika siku ya uchaguzi

**Na Beatrice Moses, TUDARCo**

KUKAMILIKA uchaguzi kuna maana nyingi. Suala la usafiri na mawasiliano bado ina nafasi yake. Katika nafasi ya pekee ndiko kunajitokeza nyenzo za usafiri barabarani, ambazo nazo katika upande wa pili wa shilingi kuna kinachowezesha usafiri huo, nyenzo mafuta.

Kuelekea kampeni za wiki ijayo, Oktoba 28, wanasiasa ndiyo wametingwa na pilikapilika kwenye majukwaa, katika harakati zao za kujinadi kwa wapiga kura katika maeneo tofauti nchini.

Ni wazi wanasiasa wanamudu kuhama kutoka eneo moja hadi jingine, wakitumia vyombo vya usafiri kama magari na pikipiki.

Vivyo hivyo, wapiga kura katika baadhi ya maeneo wamekuwa wakitumia vyombo vya usafiri kufuata na kusikiliza mikutano ya wagombea, hata wakapata mwongozo wanaomhisi atawaletea maendeleo.

Wakati wanasiasa wamekuwa wakitekeleza kampeni, kuna baadhi ya wadau zikiwamo taasisi binafsi, umma, kampuni na mashirika nao wamo.

Kampuni za mafuta nchini (OMCs) ni miongoni mwa wadau waliojitokeza kuwajibikia kampeni kuhakikisha yanapatikana kila wakati, hivyo wanaihakikishia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), upatikanaji wa petrol kipindi chote cha uchaguzi mwaka huu.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, alifanya ziara kwenye kampuni hizo kwa nyakati tofauti, alipohakikishiwa upatikanaji wa mafuta kuda wote wa uchaguzi

Mkurugenzi wa Petroli, Gerald Maganga na Meneja Biashara wa Petroli, kutoka kampuni tofauti za uuzaji mafuta, kwamba mafuta yatapatikana kwa uhakika wakati wote wa uchaguzi

Wakati nchi inaelekea kwenye uchaguzi mkuu, matumizi halisi ya mafuta ya kila siku ya dizeli katika robo ya tatu ya mwaka 2020 ilifikia lita milioni 5.83, ikiongezeka kutoka lita milioni 5.14 zilizopatikana mwaka jana; na ile ya petroli imefikia lita milioni 4.61 ikiongezeka kutoka lita milioni 3.654 zilizopatikana mwaka 2019.

Mhandisi Chibulunje, anasema kishapokea maoni kadhaa yaliyokusudiwa kuboresha usalama wa usambazaji wa bidhaa za mafuta kutoka kampuni za mafuta na pendekezo liliwasilishwa kwa EWURA kuanzisha bei ya kikomo cha chini, ili kuwalinda wasambazaji.

Anasema, EWURA na mamlaka nyinginezo husika kama Tume ya Ushindani wa BIashaera, wanalichukua suala hilo kwa uzito wake, ili liathminiwe na kuzingatiwa.

Maswala mengine ambayo yanazungumziwa ni pamoja na mikataba ya usambazaji wa mafuta ambayo wauzaji wanahitaji kuingia na wauzaji wa jumla, kufikia 30 Septemba 2020 na taarifa kwa umma za hivi karibuni zilizotolewa na EWURA zinazohitaji kwamba wauzaji wanaofanya kazi katika mikoa ya Kaskazini na Kusini kuchukua bidhaa kutoka bandari za Tanga na Mtwara.




Kituo cha mafuta kikiwa kimefungwa, aina ya huduma inapingwa hasa siku ya uchaguzi mkuu wiki ijayo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Mhandisi Chibulunje amesisitiza juu ya lengo la Serikali, pamoja na mengine, kuhakikisha usalama wa usambazaji nchini kwa kutumia bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Kampuni hizo ziliarifiwa kwamba zinapaswa kuagiza bidhaa za petroli kupitia bandari ya Tanga kuwahudumia wateja wao wanaofanya kazi katika mikoa ya Kaskazini na kupitia bandari ya Mtwara kuwahudumia wale wanaofanya kazi katika mikoa ya Kusini.

Kwa kutambua umuhimu wa uhakika wa upatikanaji wa mafuta wakati wa uchaguzi mkuu, EWURA inajikita kuhakikisha wanaweka mikakati muhimu kuhusu usambazaji mafuta kitaifa.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu huyo wa EWURA, anaeleza kuwa mwaka jana, matumizi ya petroli nchini yalikuwa wastani wa lita milioni 3.650 kwa siku na uagizaji wake tangu Januari ulizingatia wastani huo.

Anasema, kuanzia Juni iliyopita, matumizi ya petroli yaliongezeka kufikia lita milioni 3.683 kwa siku na mwezi mmoja baadaye, matumizi yaliongezeka zaidi kufikia lita milioni 4.425, wastani ni ongezeko la asilimia 21.

Mhandisi Chibulunje anasisitiza kuwa ongezeko hilo linafanya akiba ya mafuta iliyokuwepo katika maghala imeendelea kutosheleza mahitaji ya nchi, akirejea kati ya mwezi Julai 29 Julai hadi Agosti ya mwaka.

**UPUNGUFU JE?**

Mhandisi Chibulunje anasema, Kwa kiasi kikubwa upungufu katika upatikanaji mafuta ya petroli iliyojitokeza mwishoni mwa Julai iliyopita, imechangiwa na kuchelewa kwa watani wa wiki moja, meli iliyotakiwa kufike nchini kati ya tarehe 22 na 24 Julai 2020.

Anabainisha kwamba kuchelewa wa meli hiyo kulitokana na kasoro zilizokuwapo katika maandalizi ya mafuta yaliyotolewa na upepo wa kasi baharini, meli zenye mizigo kusafiri katika kasi ndogo.

"Kutokana na kuchelewa kwa meli hiyo kwa takribani siku saba, kuna uhaba kidogo uliojitokeza katika maeneo machache," anasema na kuongeza:

"Hata hivyo, EWURA ilifanya mawasiliano na kampuni za mafuta kuhakikisha mafuta yanapatikana maeneo yote."

Anasema usambazaji mafuta kwa sasa nchini ni wa kuridhisha na maeneo yote yana mafuta ya kutosha isipokuwa maeneo machache.

"Hali ya upatikanaji mafuta kwa kanda zilizo chini ya EWURA, kanda ya Mashariki inayojumuisha mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Pwani na Morogoro – mafuta yanapatikana bila matatizo," anasema.

Pia, anafafanua hali iliyopo katika kanda nyinginezo, zinazojumuisha mikoa ya Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Manyara Dodoma, Tabora, Singida na Iringa, mafuta yanapatikana pasipo walakini wowote.

Anaasema, katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inayojumuisha mikoa ya Ruvuma, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi, mafuta yanapatikana kwa kasoro uhaba ulijitokeza katika mji wa Mpanda, mkoani Katavi.

Ili kuziba pengo hili anafafanua hatia iliyochukuliwa ni kuanza kuzwa kiasi cha akiba lita 37,000 zilizoanza kuuzwa kwa wakati huo, kuna lita 100,000.

Katika Kanda ya Ziwa inayohusisha mikoa ya Mwanza, Mara, Geita, Sinyanga, Simiyu, Kagera na Kigoma, mafuta yanapatikana, isipokuwa katika wilaya za Bunda na Musoma mkoani Mara.

Ikiwa kila kukicha kunatangazwa kuiva mikakati ya kufanyika tukio hilo, hivyo kukamilika huduma ya mafuta kwa vyombo vyua usafiri, ni habari njema kuwapo uhakika wa kufanyika vyema uchaguzi na usalama.



Huduma mafuta kwa vyombo vya usafiri ikiendelea.



# H'shauri yatoa mikopo ya bil. 5/- vikundi maalum

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetoa mikopo isiyokuwa na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu Sh. bilioni 5.2 kwa kipindi cha miaka mitano.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalanganya, alisema hayo jana wakati alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha maandalizi ya tamasha la karibu Dodoma Festival kwa ajili ya kuipongeza serikali ya awamu ya tano.

Nabalanganya, alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano, makundi hayo katika Jiji la Dodoma yamenufaika kwa kupata mikopo bila riba ambayo imewawezesha kujikwamua kiuchumi.

Alisema, kipindi cha nyuma makundi ya watu wenye ulemavu yalikuwa yakiomba mitaani misaada kutokana na kukosa mitaji kwa ajili ya kuanzisha miradi.

"Mikopo hii ambayo kwa kipindi cha miaka mitano tumetoa takribani Sh. bilioni 5.2 imewezesha makundi haya kuwa na miradi ya kuzalisha ambayo imewasaidia kujiinua kiuchumi," alifafanua. Alisema, jiji hilo lilianza kutoa mikopo kwa makundi hayo rasmi mwaka 2015, kwa miaka ya nyuma ilikuwa inatoa, lakini hapakuwa na sheria ya kusimamia halmashauri kutekeleza agizo hilo la serikali. "Tunamshukuru sana Rais Magufuli, alipoingia madarakani pakawapo na mchakato wa kutengeneza sheria hii, lakini pia kundi la watu wenye ulemavu ambalo halikuwapo awali likaingizwa kwa mujibu wa sheria na wao hivi sasa wanapata asilimia mbili ya mikopo," alisema. Pia, alisema kuwa mwezi huu wanatarajia kutoa kiasi cha Sh. milioni 545, bodaboda 46 na bajaji 21 kwa vijana 67.

"Tumeamua kutoa mikopo ya pikipiki pia kwa vijana ili kuwaondolea adha ya mikopo ya pikipiki za mkataba kwa watu binafsi, ambayo imekuwa ikiwagharimu kwa pikipiki moja hadi shilingi milioni nne," alisema. Akizungumza kwa niaba ya vijana wanufaika wa mikopo ya halmashauri, katibu wa umoja wa vikundi vya wenye ulemavu, vijana na wanawake, Christopher Dioniz, alisema wanaishukuru serikali kwa mikopo bila riba.

Alisema wao kama vijana wamenufaika na mikopo hiyo ambayo imewawezesha kuanzisha miradi ya ufugaji kuku na hivi sasa wanazalisha vifaranga, mayai pamoja na kuku wa nyama.

"Sisi kikundi chetu tulipatia kiasi cha Sh. milioni 30 ambazo tutarejesha bila riba hivyo tunaishukuru serikali kwa kuwa hali hii hakuna kijana kati yetu ambaye anatamani tena kuajiriwa kwa kuwa fedha tunazopata ni zaidi ya mshahara wa mtumishi wa umma," alisema.

Mratibu wa tamasha hilo, Simon Mwapagata, alisema lengo ni kumpongeza Rais Magufuli kwa kusaidia makundi yote katika kipindi cha miaka mitano ya utawala wake.

"Tamasha hili ambalo siyo la kisiasa, litafanyika Oktoba 24, mwaka huu katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma na mgeni rasmi atakuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, wageni wengine ni pamoja na msemaji mkuu wa serikali Dk. Hassan Abbas," alisema.



Mwendesha guta akiwa amepakia mzigo wa miwa na abiria wawili juu barabara kuu ya Dodoma-Morogoro, eneo la Kibaigwa, Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CPB yatafuta kampuni za nje kununua mazao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAIMU Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Valerian Mablangeti, amesema wanaendelea na mazungumzo na kampuni za nje ya nchi kwa ajili ya kuingia mkataba wa kuyauzia mazao yao.

Akizungumza jana jijini hapa na waandishi wa habari alisema, mazao ambayo wanatarajia kuanza kuyauza nje ni pamoja na korosho, maharagwe mabichi, ufuta, maharagwe ya soya na viungo.

Mablangeti, alisema kuwa fursa hizo zote zinalenga kumpa uhakika wa soko mkulima wa Tanzania. "Iko miradi mingi inayoendelea maeneo mengine ikiwa ni pamoja na kilimo cha mkataba cha muhogo kwa ajili ya kuuza nchini China," alisema Mablangeti. Alisema, matarajio ya mradi huo ni kuuza tani 1,200,000 kwa mwaka ndani ya miaka mitatu ijayo na usajili wa wakulima unaendelea mkoani Mtwara.

Pia, alisema hivi sasa bodi hiyo imeagiza mashine zenye uwezo wa kukoboa tani 96, za mpunga kwa siku.

"Mitambo hiyo itasimikwa eneo la Mbuyuni, jijini Mwanza na inatarajia kuwasili nchini mwanzoni mwa mwezi Desemba 2020," alifafanua.

Alisema, kutokana na kusimikwa kwa kiwanda hicho, CPB imeanzisha vituo vya ununuzi wa mpunga kwenye ghala zake jijini Mwanza, pia vituo vya ununuzi mjini Mpanda na Kahama na mahitaji ya kiwanda ni tani 29,000 kwa mwaka.

"Kule mkoani Kigoma, bodi inatarajia kufungua mitambo ya kuchakata muhogo kwa ajili ya viwanda vyake," alisema.

Vile vile, alisema kuwa bodi hiyo imeanzisha kiwanda kidogo cha kukaanga na kuuza korosho na karanga za kukaanga pamoja na siagi ya mazao hayo.

Alisema, lengo ni kuongeza thamani na kutengeneza ajira zaidi nchini kama ilivyo azma ya serikali ya awamu ya tano.

Alisema kuwa bodi inafanya mazungumzo na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Magereza ili kuingia mikataba ya kilimo cha alizeti kwa ajili ya kiwanda chake kilichopo Dodoma chenye uwezo wa kuchakata tani 6,000 kwa mwaka.

Hata hivyo, aliwataka wadau wengine wa sekta ya nafaka na mazao mchanganyiko kushirikiana kuhakikisha malengo na mipango ya CPB, inafikiwa na kuleta matokeo yanayokusudiwa.

# DUWASA kutoa maji Ziwa Victoria

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Dodoma (DUWASA), inatarajia kuanza kutoa maji Ziwa Victoria kuja katika mkoa wa Dodoma ili kukabiliana na upungufu wa huduma hiyo.

Pia, DUWASA itaendelea na miradi ya uboreshaji maji katika maeneo tofauti ikiwa ni jitihada za kufikisha maji kwa kila mtu mwenye uhitaji.

Akizungumza na Nipashe Mkurugenzi wa DUWASA, David Pallangyo, alisema lengo la kufanya hivyo ni pamoja na kutaka kila kona ya jiji hilo kuwa na maji ya kutosha.

Hata hivyo, alisema wamefanikiwa kuchimba visima vya maji vitano ambavyo vina uwezo wa kuhudumia watu wasiopungua 600, kwa kila kisima kimoja.

Alisema mkataba walioingia DUWASA na DDCA ambao wapo chini ya Mamlaka ya Majisafi Vijijini (RUWASA) ni kuchimba visima 10.

Alifafanua kuwa lengo la kuchimba visima ni kutaka kuongeza upatikanaji wa maji jijini hapo na kuna ongezeko la wakazi kulingana kutoka na ujio wa makao makuu.

Pallangyo, alisema visima hivyo vina uwezo wa kutoa lita 65,000 kwa saa kwa kila kimoja na kutosheleza mahitaji katika eneo lililopo kisima.

Alisema huo mpango wa uchimbaji visima ni endelevu lengo ni kulifanya jiji kuwa na maji ya kutosha.

Pia alisema visima vimeshachimbwa katika maeneo tofauti, ili kukidhi mahitaji ya maji kwa wakazi wa maeneo mbalimbali jijini hapo.

"Dodoma itazidi kuwa na maji kwa sababu DUWASA ina mikakati ya muda mrefu kuboresha mifumo ya maji," alisema Pallangyo.

Alisema wanatarajia kuanza kutoa maji eneo la Ihumwa kuleta mjini ili kuongeza huduma hiyo na kumaliza kero ya huduma hiyo kwa watu.

Kadhalika, alisema serikali ipo makini katika sekta ya maji ndiyo maana kila kukicha wamekuwa wakiboresha mifumo ya maji katika maeneo mbalimbali nchini.

Aliwata wananchi kutokuwa na wasiwasi juu ya upatikanaji wa huduma ya maji jijini hapo kwa kuwa hivi sasa mifumo imeshaboreshwa.

Akizungumzia kuhusu mradi wa maji wa Farkwa, alisema kila kitu kipo tayari wanasubiri tenda ili uunganishwaji maji uendelee katika chanzo hicho.

Alisema, miradi ya maji itaendelea kuboreshwa ili kuhakikisha yanapatikana kwa wingi.

Aliwataka wakazi wa maeneo mbalimbali kutunza vyanzo vya maji kwa sababu huduma hiyo ni muhimu kwa afya ya binadamu.





# Mjane arejeshewa nyumba iliyouzwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya imeokoa na kuirejesha nyumba ya mjane, Naijeria Ngogo, Mkazi wa Kijiji cha Mpakani katika Kata ya Ubaruku wilayani Mbarali ambayo ilikuwa imeuzwa na kampuni inayotoa mikopo umiza.

Akizungumza na waandishi wa habari ofsini kwake, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, alisema nyumba ya mama huyo ina thamani ya Sh. milioni 1.5 na iliuzwa na kampuni ya ukopeshaji ya Yuan Credit.

Kampuni hiyo, alisema ilimkopesha mama huyo Sh. 500,000 kwa riba ya Sh. 100,000 na hivyo alitakiwa alipe Sh. 600,000 ambazo baada ya kushindwa kulipa, kampuni hiyo iliiuza kwa Sh. 600,000.

"Huyu mama alikopeshwa fedha hizo Agosti 4, mwaka huu, kwa makubaliano ya kulipa ndani ya mwezi mmoja na wakati nyumba yake inauzwa alikuwa ameshalipa Sh. 195,000. Tulibaini kuwa kampuni hiyo iliuza nyumba ya mama huyo kabla ya muda waliokubaliana kuisha," alisema Matechi.

Alisema TAKUKURU iliirejesha nyumba hiyo kwa mjane huyo na kumrejeshea fedha mtu aliyekuwa ameinunua nyumba hiyo na kumaliza mgogoro huo.

Hata hivyo alisema waliamua kuirejesha nyumba hiyo baada ya mjane huyo kumaliza kulipa mkopo wake kwa kulipa Sh. 405,000 na hivyo mgogoro ukawa umeisha.

Aliwataka wananchi kuepuka kukopa mikopo kwenye taasisi hizo na badala yake waende kwenye taasisi za fedha hasa benki ambako kuna usalama zaidi.

# Wagombea walioenguliwa wazua tafrani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAFRANI imeibuka jijini hapa wakati wa kuwaapisha mawakala wa vyama vya siasa watakaosimamia uchaguzi mkuu baada ya wagombea udiwani 16 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) walioenguliwa kujitokeza kuapa.

Watu hao walizua tafrani juzi kwenye ukumbi wa Shule ya Sekondari Mbeya ambako mawakala na wagombea udiwani walikuwa wanaapishwa huku wakidai kuwa hawajawahi kukabidhiwa barua na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwa wameenguliwa kugombea nafasi hizo.

Mmoja wa wagombea udiwani hao, Saada Adam, kutoka Kata ya Maanga, alisema wana haki ya kushiriki kwenye uchaguzi kwa sababu hawana barua zozote ambazo zinawaelekeza kuwa hawastahili kushiriki.

Alisema yeye ni miongoni mwa wanawake wachache waliokuwa wamejitokeza kuomba ridhaa ya wananchi kuchaguliwa kuwa madiwani, lakini anasikitika kuenguliwa huku akidai kuwa kinachotendeka ni hujuma dhidi yao.

"Kwa nini waapishwe wengine halafu sisi tuzuiwe wakati tume haijatukabidhi barua za kuzuiwa kushiriki. Mimi naamini kuwa hizi ni hujuma za kutaka kutudhoofisha, lakini hawataweza," alisema.

Naye Abdulkarim Juma, aliyekuwa mgombea udiwani wa Kata ya Sisimba, alisema ana wasiwasi kuwa kuzuiwa kwao ni mbinu za Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Mbeya Mjini kutaka kuwahujumu.

Alisema chama hicho hakitakubali kuhujumiwa na badala yake watapambana kuhakikisha haki yao inapatikana ili kuepusha migogoro zaidi.

Katika hatua nyingine, mawakala wa Democratic Party (DP) walilalamika kuwa walizuiwa na Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Mbeya kuapa kwa madai kuwa barua zao hazikuwa na anwani wala nembo za chama chao.

Katibu wa DP Mkoa wa Mbeya, Nicodemus Ngwala, alisema uamuzi wa msimamizi huyo wa uchaguzi si sahihi kutokana na ukweli kwamba chama hicho kina mgombe urais ambaye atatakiwa kupigiwa kura na wananchi wa Jiji la Mbeya.

"Tukizuiwa sisi tafsiri yake ni kwamba mgombea wetu wa urais hatakuwa na mawakala kwenye vituo vyote 260 vya Jiji la Mbeya kitu ambacho si sahihi kwa mujibu wa sheria na kanuni za uchaguzi mkuu," alisema Ngwala.

Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Mbeya Mjini, Amede Ng'wanidako, alisema yeye alikabidhiwa orodha ya wagombea udiwani 20 pekee wa jiji hilo na hao 16 walikuwa tayari walishaenguliwa kwenye mchakato huo.

Alisema alishawakabidhi barua za kuenguliwa wagombea hao na kwamba alipokuwa anawakabidhi walitia saini kwenye kitabu cha kupokelea vitu (dispatch) na hivyo hawezi kuwaapisha.

"Lakini hawa mawakala wa DP nimewazuia kuapishwa kwa sababu barua zao hazina anwani wala nembo ya chama chao kama ambavyo sheria na kanuni za uchaguzi zinaelekeza," alisema Ng'wanidako.

Mawakala wa vyama vya siasa, wagombea udiwani na ubunge wa vyama mbalimbali walianza kuapishwa juzi na kutokana na mamlaka iliyo nayo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iliongeza siku tatu ambazo zinamalizika leo.



Mkuu wa Idara ya Uhamiaji wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhamiaji, Msafiri Shomari, akiwaonyesha waandishi wa habari jana, nakala ya hukumu ya raia wa Malawi, aliyekamatwa akiwa na kitambulisho cha mpigakura kilichotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC). **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Raia Malawi atozwa faini mil. 100.6/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MTU mmoja, raia wa Malawi aliyekamatwa hivi karibuni mkoani Mbeya akiwa na kitambulisho cha mpigakura kilichotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) pamoja na fedha za kigeni bila kuzitolea taarifa, ametozwa faini ya Sh. milioni 100.6 kutokana na makosa matatu aliyoshtakiwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake baada ya kupokea nakala ya hukumu kutoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhamiaji Mkoa wa Mbeya, Msafiri Shomari, alimtaja mtu huyo kuwa ni Tedy Mwaisemba.

Shomari alisema mtu huyo alipolipa faini hiyo aliachiwa huru na kuruhusiwa kurudi nchini kwao ambako ndiko anafanyia biashara zake ambazo bidhaa nyingi anazitoa Tanzania.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa Machi, mwaka huu na maofisa wa Idara ya Uhamiaji kwa kushirikiana na maofisa wa vyombo vingine vya dola kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) wakati akijiandaa kusafiri kwenda jijini Dar es Salaam. Alisema baada ya kupekuliwa, maofisa hao walibaini kuwa alikuwa ameingia nchini isivyo halali kutokana na nyaraka alizokuwa nazo. Pia alikutwa na Dola 30,000 ambazo alikuwa hajazitolea taarifa pamoja na kitambulisho cha mpigakura cha Tanzania.

Shomari alisema katika kosa la kwanza la kuingia nchini isivyo halali, ametozwa faini ya Sh. 500,000, kosa la pili la kuingia na fedha za kigeni ametozwa faini ya Sh. milioni 100 na kosa la kukutwa na kitambulisho cha mpigakura cha Tanzania ametozwa Sh. 100,000.

"Tunashukuru kwamba kesi hii imemalizika vizuri mahakamani kwa kuwa mtuhumiwa ameadhibiwa kwa kulipa faini ya Sh. milioni 100.6 ambazo amezilipa na kuachiwa huru na hili ni fundisho kwa wageni wengine wanaoingia nchini," alisema Shomari.

Alisema historia ya mtu huyo inaonyesha kuwa alikuwa raia wa Tanzania, lakini aliamua kuukana utanzania na akaomba uraia wa Malawi, hivyo kwa sasa hana haki ya kuhudumiwa kama Mtanzania na badala yake anahudumiwa kama mgeni. Ofisa huyo aliwashauri raia wengine wa kigeni wanaoingia Tanzania hasa kupitia kwenye mipaka ya Mbeya kuhakikisha wanafuata taratibu za uhamiaji ili kukwepa mkono wa sheria kama uliomkumba Mwaisemba.

"Nawaomba Watanzania ambao wana ndugu zao walioukana utanzania kuhakikisha wanafuata sheria za nchi, na ningewashauri sana Watanzania wasipende sana kuukana utaifa wao na kung'ang'ania uraia wa mataifa mengine," alisema Shomari.

# Balozi Iddi ahamasisha vijana kuchangamkia fursa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amewataka vijana kuchangamkia fursa mbalimbali za mafunzo ya amali (ufundi), zinazotolewa na ikiwa ndio njia pekee ya kuwakomboa na tatizo la ajira liliopo nchini.

Alisema uchangamkiaji huo wa fursa za mafunzo ni vyema ukienda na jitihada za wazazi na walezi kuwashajiisha vijana kujiunga na mafunzo ya amali kwa manufaa ya maisha yao ya baadaye na taifa kwa ujumla.

Akizungumza na vijana waliohitimu mafunzo ya ujuzi wa ufundi katika vyuo vya ufundi kwa Unguja na Pemba kwa mwaka 2020, Kikwajuni, Balozi Iddi alisema mhitimu wa vyuo hivyo ana nafasi kubwa ya ajira akilinganishwa na yule anayetoka chuo kikuu ambaye inampasa apambane kutafuta kazi.

Alisema Dira ya Maendeleo Zanzibar ya mwaka 2000 hadi 2020 iliweka shabaha ya kuongeza ajira kwenye sekta ya utalii, kilimo na nyingine.

Balozi Iddi alieleza kwamba shabaha hiyo imekusudia kupunguza kiwango cha ukosefu wa ajira kutoka asilimia 17.1 hadi kufikia asilimia 10, ili pia kuongeza uwezo wa watendakazi kwa nia ya kuchukua fursa za ajira pale zinapojitokeza.

Alisema katika kuufanyia kazi mwongozo wa taifa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilianzisha programu ya ajira kwa vijana inayowaongoza kubaini mahitaji yao wenyewe kwa sekta za uzalishaji kama kilimo, uvuvi, ufugaji, uhunzi, na kazi za sanaa na michezo.

"Ikishabainika mahitaji yao kinachofuata ni kuwajengea uwezo wa kiufundi ili kukabiliana na fursa katika soko la ajira nchini na hata kimataifa," alisema Balozi Iddi.

Alisema sera za kitaifa na kisekta zilizopo zinaonyesha jinsi Zanzibar ilivyolichukulia suala la ajira kwa vijana kuwa ni jambo la msingi na muhimu linalohitaji kufanyiwa kazi kwa umakini mkubwa.

Alisema kwa vile serikali imeshatekeleza jukumu lake kwa kuwapatia mafunzo vijana hao, kinachofuata hivi sasa ni kuchapa kazi kwa mujibu wa fani walizosomea.

Akitoa taarifa ya mafunzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Bakari Ali Silima, alisema jumla ya vijana 660 kutoka wilaya zote za Zanzibar, walishiriki mafunzo hayo yaliyolenga kuwapatia ujuzi wa kukidhi mahitaji yao ya kimaisha.

Alisema uimarishaji wa mafunzo ya ufundi chini ya mamlaka ya mafunzo ya amali Zanzibar, umejikita katika mfumo wa mabadiliko ya uchumi wa viwanda kupitia mafunzo ya ufundi wa vifaa vya umeme, ushonaji, upambaji na uselemala.

Alisema katika kuimarisha uwezo wa vijana wanaomaliza masomo yao, mamlaka ya mafunzo ya amali imeongeza programu mpya mwaka ujao katika fani ya uvuvi kwa vile taifa tayari limeshajielekeza katika uchumi wa bluu.

Hata hivyo, Dk. Bakari alisema, zipo baadhi ya changamoto zilizokwaza wanafunzi hao katika mafunzo yao akizitaja kuwa pamoja na kuzuka kwa ugonjwa wa corona, utoro kwa baadhi ya wanafunzi pamoja na ongezeko kubwa la wanafunzi lililosababisha kukaa nyumbani.



Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Raymond Mwangwala (katikati), akiwanadi wagombea ubunge Jimbo la Mfenesini Zubeda Khamis (kushoto) na mgombea uwakilishi Jimbo la Mfenesini, Machano Said, wakati akifunga kampeni za jimbo hilo, mkoa wa Mjini Magharibi Unguja juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZEC yabandika orodha wapigakura Okt. 27, 28

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imebandika Daftari la Kudumu la Wapigakura katika maeneo yote 407 yatakayotumika kwa upigaji kura wa mapema wa Oktoba 27 na upigaji kura wa pamoja utakaofanyika Oktoba 28, Unguja na Pemba.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati alipotembelea kituo cha kupigia kura cha Shule ya Mwembe Shauri, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Thabit Idarous Faina, alisema hatua hiyo itawasaidia wapigakura kujua taarifa zao na vituo vyao vya kupigia kura kabla ya siku ya kupiga kura.

Mkurugenzi Faina, alieleza kuwa, Tume imebandika daftari hilo kwa maeneo yote ya kupigia kura ikiwa ni maelekezo ya kifungu cha 39 cha Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar namba 4 ya mwaka 2018 ambacho kinamtaka msimamizi wa uchaguzi kubandikia daftari la wapigakura katika sehemu ya wazi ya eneo la kupigia kura siku saba kabla ya upigaji kura.

"Kifungu cha 39, msimamizi wa uchaguzi atabandika, siku saba kabla ya upigaji kura daftari katika sehemu ya wazi ya eneo la kupigia kura ili kuwezesha wapigakura kufahamu taarifa zao na vituo vya kupigia kura," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema, Tume imeweka utaratibu maalum ambao utamrahisishia zaidi mpigakura kujua taarifa za eneo na kituo cha kupigia kura kwa kutumia simu ya mkononi kupitia mtandao wa Zantel na anaweza kubonyeza alama ya nyota *152*29#.

Akizungumzia kuhusu orodha ya wapigakura ya mapema alisema kuwa orodha hiyo pia imebandikwa katika maeneo hayo kama kanuni zinavyoelekeza na kuwataka wapigakura hiyo ya mapema na wa Oktoba 28 kwa kura ya pamoja kutumia fursa hiyo kwenda kuangalia majina yao ili waepuke usumbufu siku ya kupiga kura.

# Maalim Seif amaliza kifungo cha kampeni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BAADA ya kumaliza siku tano za kufungiwa kutofanya kampeni, mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, alisema endapo atapata ridhaa ya Wazanzibari atahakikisha kila nyumba ya mwananchi wa Zanzibar inakuwa na huduma ya majisafi na salama.

Aliyasema hayo huko katika Viwanja vya Garagara, Unguja Mjini katika mkutano wake wa hadhara ikiwa ni sehemu ya kampeni zake za urais.

Alisema anashaangaa kuiona Zanzibar haina maji wakati imezungukwa na maji na kudai atahakikisha huduma hiyo inawafikia wananchi wote.

"Sitaki kusikia kuwa kuna Mzanzibari ambaye hapati huduma ya majisafi, nitapambana kwa nguvu zote," alisema Maalim Seif.

Alisema atahakikisha shirika ambalo linashughulikia huduma ya maji analifanyia mabadiliko makubwa ili liendane na wakati.

Pia, akizungumzia suala la umeme alisema atahakikisha Zanzibar inakuwa na vyanzo vyake na kuachana na kutegemea vyanzo vya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

"Nitahakikisha tunakuwa na vyanzo vyetu vya umeme ili tuufanye umeme uwe wa bei nafuu na kila mwananchi aweze kuutumia," alisema Maalim Seif.

Alisema pia anakusudia kufanya umeme kuwa wa bei nafuu ili ushawishi kuwavutia wawekezaji waingie Zanzibar kuwekeza viwanda vidogo na vya kati na kuongeza nafasi za ajira.

"Umeme ukiwa rahisi basi utaona wawekezaji watakavyoingia kwetu, hapo utaona raha ya umeme wa bei nafuu," alisema.

Kwa upande wa nyumba za kisasa, alisema akiingia madarakani atawajengea wananchi wake nyumba za bei nafuu zenye kiwango vizuri.

Alisema ataanzisha shirika maalum la kushughulikia ujenzi wa nyumba za kisasa na kuwaelekeza nyumba itakayojengwa ikikamilika anapewa mwananchi.

Pia, alisema katika kukamilisha hilo atakaribisha kampuni ya kufanya kazi hiyo na baadaye watarudishiwa fedha zao kwa awamu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA NA MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA IKO KAHAMA** MAJENGO VYUMBA VITATU INA MAJI NA UMEME, PLOT No 759, BLOCK "E", KIWANJA NI MEDIUM SIZE. MAWASILIANO ZAIDI; 0759359933/0713553819

**NIPASHE NI JIBU LAKO**
**NJOO UTANGAZE NASI**
**KWA BEI NAFUU SANA**
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTOLEWA KWA KADI YA BAJAJI

**STANSLAUS BERNARD KWIMENYA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 997 ALD** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa
**WMB/RB/1052/2020**

115955401

## KUITWA SHAURINI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGRO.**

MAOMBI NA.260 YA MWAKA 2020.

**RAMADHANI HEGA**...............MLETA MAOMBI

DHIDI YA
**POWA NOFELI**.............................MJIBU MAOMBI

WITO/KUITWA SHAURINI KWA

**POWA NOFELI**
Popote Ulipo Unaarifiwa Ufike katika baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe **05/11/2020** wewe mwenyewe binafsi au mtume wawakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hamtoudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

**Imetolewa kwa mkono wangu leo tarehe 07 Mwezi October,2020.**

215956202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATHEW ALBERT MBWANA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **MAZDA -STATION WAGON** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 112 BJF.** CHASSIS NAMBA **DW5W402059.** ENGINE NAMBA **B5504511.** YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI:
**DAR/CHA/RB/750043/2020**

215955902

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;316/2020**
Ombi la **JUMA KULUJAKAYA HASSAN** ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SHOMARI RAMADHANI SALUM.**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **20/10/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **20/10/2020.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;325/2020**

**Ombi la HALIMA AYUBU ABDALLAH ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu REHEMA VINCENT DIMOSSO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 03/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 22/10/2020.

115956102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MKUMBURU**
**Wilaya HANDENI**
**MADAI NAMBARI 29 YA 2020**

Mdai: **SYLVESTER ALFRED MKOLE**
Mdaiwa **HAMISI S/O SHIMBI (MIZENGO)**
Kwa: HAMISI SHIMBI (MIZENGO)
Kwa kuwa mdaiwa/mdai/ameleta/wameleta /madai yake/yao kwamba
Mnamo mwezi **2/2011** ulimkabidhi gari mdai kwa ajili ya matengenezo kwa makubaliano ya malipo ya **Tsh. 700,000/-** na ukamlipa **Tsh. 660,000/-** kisha ukalitelekeza gari hilo. Hivyo unadaiwa **Tsh. 40,000/-** za matengenezo na gharama za ulinzi **Tsh. 3,450,000/-** jumla Tsh. **3,490,000**
**(Milioni tatu laki nne na tisini elfu tu.)**
Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe **8/12/2020** saa **2:30 asubuhi** kwa kujibu madai hayo, na kwakuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo, lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri ya Mahakama hii leo tarehe **20/10/2020.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **MUSHOBOZI COSTANTIN NDIBALEMA** amepotelewa na kadi ya pikipiki aina ya Bajaj yenye namba za usajili **MC 553 AHA.** taarifa polisi RB Namba **KAG/BUK/RB/725902/2020.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au awasiliane na mhusika kwa namba **0627003551.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**W S INSIGHT** wanatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN HARDBODY** zenye namba za usajili **T 363 DDX** kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Polisi taarifa
**DAR/OST/RB/736653/2020**

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;319/2020**
Ombi la **LAMECK JULIUS MWAKALINGA** ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **JULIUS LAMECK MWAIPAJA.**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **18/12/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **21/10/2020.**

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;320/2020**
Ombi la **NDENI RAY MWASHA** na **ROMEO RAY MWASHA** ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **AMINIUFOO HEZEKIEL MURO.**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **27/10/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **21/10/2020.**

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;294/2020**
Ombi la **ZAWADI OTHUMANI NDEHANDE** ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **JALIA SALUM LUPAPULO.**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 08/12/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **05/10/2020.**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Wahariri waombwa kuunga mkono huduma bima ya afya

**Na Hellen Mwango, DODOMA**

WAHARIRI wa vyombo vya habari nchini wametakiwa kuunga mkono juhudi za serikali katika mpango wa huduma mbalimbali za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ili kuondoa taarifa za upotoshaji na sizizo za kweli.

Kadhalika wametakiwa kubeba taarifa za kweli na kutoa mrejesho wa hali halisi ya upatikanaji sahihi wa huduma za NHIF kwa jamii.

Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Edward Mbanga, alitoa rai hiyo jana wakati akifungua mkutano wa wahariri wa vyombo kuhusu uboreshaji wa NHIF jijini Dodoma.

"Nawaomba wahariri kuunga mkono juhudi za serikali ili kuondoa upotoshaji, zisizo za kweli kuhusu upatikani huduma kupitia NHIF, bebeni taarifa za kweli, mtoe mrejesho halisi kwa jamii," alisema Mbanga.

Alisema si rahisi wananchi kunufaika na maboresho ya sekta ya afya kama wahariri hawapati taarifa sahihi za mfuko.

Pia alisema serikali inaendelea na mkakati wa kuboresha huduma za afya kwa wananchi wasio na uwezo kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anahudumiwa kupitia NHIF.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema wahariri ni kiungo muhimu kwa kutoa elimu kuhusu mfuko ili kuwa na uelewa zaidi.

Alisema vyombo vya habari ni sehemu ya NHIF ikiwamo kusaidia kufanya tafiti za kihabari katika kuboresha na kuchochea huduma bora kwa jamii kuhusu umuhimu wa bima ya afya.

# Wanafunzi wanaoshiriki ngono wadaiwa kupungukiwa umakini

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

WANAFUNZI wanaojihusisha na vitendo vya ngono wanapungukiwa umakini katika masomo yao, hivyo kuwafanya washindwe kufaulu mitihani yao, imeelezwa.

Kadhalika, imeelezwa kuwa mimba za utotoni, kushuka kwa nidhamu kwa wanafunzi na wazazi kutofuatilia maendeleo yao huchangia kushuka kiwango cha elimu.

Kauli hiyo ilitolewa jana mkoani Mwanza katika kikao Cha wadau wa Elimu na

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mwanza, Martine Nkwabi, alisema hayo jana katika kikao cha wadau wa elimu kilichofanyika jijini hapa huku akibainisha sababu zingine za kushuka kiwango cha elimu kuwa ni mazingira ya shule kuwa mbali pamoja na kuporomoka kwa maadili miongoni mwa walimu.

Alisema takwimu za mamlaka za serikali zinaonyesha katika shule za msingi kuanzia mwaka 2015 hadi 2019, wanafunzi waliosajiliwa walikuwa 462,235 lakini waliomaliza ni 312,545.

Kwa upande wa shule za sekondari kuanzia mwaka 2016 hadi 2019 waliosajiliwa walikuwa 158,257 huku waliomaliza wakiwa 102,935 na walioacha ni 55,322.

"Walimu baadhi hushiriki udanganyifu kwenye mitihani ya taifa, kuwatumia wanafunzi kingono, upungufu wa walimu , upungufu wa miundombinu na samani na umbali kati ya shule na makazi, huchochea wanafunzi kukatisha masomo.

"Jambo hilo huongeza tabaka la watu wajinga na wahalifu na pia hushusha asilimia ya ufaulu wa shule na kuvuruga malengo ya taifa," alisema.

Aliongeza kwa ili kuondokana na adha hizo mikakati mbalimbali ya kupandisha taaluma imeandaliwa ikiwamo kudhibiti utoro na mimba shuleni kwa kuanzisha vipindi vya dini na ushauri nasaha.

Jitihada zingine alizitaja kuwa ni kila halmashauri kuunda kamati ya maendeleo ya elimu kata ( KAMAEKA), wazazi kuwa sehemu muhimu ya kuwaendeleza watoto wao kitaaluma.

Pia alisema serikali imeanza kudhibiti utoro wa walimu na maombi ya ruhusa zisizo na tija, kutopoteza kipindi chochote kwenye darasa, kuwapo kwa program za ufundishaji wa ziada unaozingatia uwezo wa wanafunzi.

Alisema halmashauri pia zinafanya vikao na maofisa elimu kata na walimu wakuu kila mwezi na kuwapo utaratibu wa kuaminika wa ufatiliaji wa ufundishaji kwenye shule zote zilizopo kwenye kila halmashauri.

Mwenyekiti wa kikao hicho, ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Cornel Magembe, alisema ni jambo la aibu kila yanapotoka matokeo ya kitaifa na Mkoa wa Mwanza unakuwa uko chini.

Alisema yote hayo yanasababishwa na ufuatiliaji na usimamizi kutokuwa mzuri, hivyo aliiagiza ufatiliaji uwe mkubwa ili kuleta maendeleo katika sekta hiyo ya elimu.

# Wafanyabiashara waomba elimu kodi

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

WAFANYABIASHARA katika soko la dhahabu wilayani hapa, wameiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Kikodi wa Kahama kuendelea kutoa elimu endelevu kwa makundi ya walipakodi kuhusu matumizi sahihi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki (EFD).

Kwa kutoa mafunzo hayo mara kwa mara, wamesema kutaondoa mianya ya rushwa inayoweza kutokea kwa kampuni za hesabu.

Hayo yalisemwa juzi na wafanyabiashara wa soko la ununuzi wa dhahabu wilayani Kahama wakati wakizungumza na waandishi wa habari kuhusu vikwazo ambavyo wamekuwa wakizipata katika biashara hiyo ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi ya mashine hizo.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara hao, Mwenyekiti wa Soko hilo, Emmanuel Kidenya, alisema kuwapo kwa mashine hizo kutasaidia kutunza kumbukumbu zao za mwaka na kutengeneza hesabu nzuri za kodi, hivyo kuondoa usumbufu kwa mamlaka husika.

Kidenya alisema kwa kutumia mashine hizo, kutarahisisha wafanyabiashara kujua faida na hasara na kuepuka kulipa kodi zaidi au pungufu kwa mamlaka husika, hivyo kuondoa usumbufu.

"Kwa kutumia mashine za EFD kutaondoa changamoto ya kukadiriana bila kujua hesabu kamili inayotakiwa kulipwa kwa kuwa hesabu zetu tutakuwa tukijitengenezea wenyewe bila kutumia kampuni za hesabu zilizopo sasa," alisema.

Meneja wa TRA Mkoa wa Kahama, Warioba Kanire, aliwataka wafanyabiashara wa soko la dhahabu kuwa wepesi katika kutunza kumbukumbu zao za mauzo pamoja na ununuzi wa bidhaa zao zitakazosababisha ukokotoaji wa kodi unaoendana na hali halisi ya biashara hiyo.

Meneja huyo alisema wameamua kutoa elimu juu ya matumizi ya mashine hizo ili kuwasaidia wafanyabiashara katika kijitambua nini wafanye katika biashara kwa kutumia mashine hizo.

Alisema kwa kuzingatia biashara ya madini inavyofanyika katika soko la madini lililopo mjini Kahama, Warioba aliwasihi wafanyabiashara hao kujitokeza kwa wingi kuendelea kutumia mashine hizo kwa usahihi na kutunza kumbukumbu za biashara zao ili iwe rahisi kwao kujua faida inayotokana na biashara wanaoifanya.


**BANI INVESTMENT LIMITED**

**TANGAZO LA MNADA**

| JINA LA MDAIWA | MALI ILIYOWEKWA DHAMANA | MAHALI ILIPO | TAREHE | MUDA |
|---|---|---|---|---|
| KORU FREIGHT LIMITED/ PETER LEINA ASSENGA | Nyumba ya biashara (guest house/hostel) yenye CT No. 52152, L.O Na. 191258, Kitalu Na."C" Kiwanja Na.238/1. SQM 655 | Kunduchi Mtongani karibu na CCM,Dar es salaam | 7.11.2020 | 4:00 asubuhi nakuendelea |
| KORU FREIGHT LIMITED/ PETER LUCAS ASSENGA | Nyumba ya kuishi yenye CT No. 56155, L.O Na. 213224, Kitalu Na."B" Kiwanja Na.1197. SQM 825 | Ubungo Kibangu,Dar es salaam | 11.11.2020 | 4:00 asubuhi nakuendelea |
| KORU FREIGHT LIMITED/ PETER LEINA ASSENGA | Nyumba ya kuishi yenye CT No. 55761, L.O Na. 213077, Kitalu Na."D" Kiwanja Na.404. SQM 110 | Mabibo relini,Dar es salaam | 11.11.2020 | 6:00 mchana nakuendelea |
| KORU FREIGHT LIMITED/ PETER LEINA ASSENGA | Nyumba ya kuishi yenye CT No. 114650, L.O Na. 395187, Kitalu Na."Q" Kiwanja Na.10 SQM 4,614 | Luguruni,Dar es salaam | 14.11.2020 | 4:00 asubuhi nakuendelea |

Kwa idhini tuliyopewa na Benki ya **NCBA Tanzania,** tutauza kwa mnada wa hadhara mali zilizowekwa kama dhamana ya mkopo. Mnada utafanyika mahali zilipo mali hizi, siku na saa kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**MASHARTI YA MNADA**

1. Nyumba zitauzwa "kama zilivyo " ***as is where is basis***"
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na 75% katika muda wa siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Ofisi ya:

**BANI INVESTMENT LTD, P.O. Box 71340 Dar es Salaam LIDA Building 3rd floor office No. 0313 Nkrumah Street Tel: 0713 224 578, 0718 384 796**



**KUMBUKUMBU**



TAREHE 23/10/2018 UMETIMIZA MIAKA MIWILI (2) SASA TANGU UITWE NYUMBANI KWA BWANA INGAWA BABA YETU HAUPO NASI KIMWILI LAKINI KIROHO TUPO PAMOJA KATIKA SALA NA MAOMBI ULIKUWA NGUZO IMARA KATIKA MAISHA YETU, HEKIMA NA BUSARA ZAKO TUNAZIKUMBUKA DAIMA. TUNASHUKURU MWENYEZI MUNGU KWA MAISHA YAKO KWETU HAKIKA PENGO ULILOLIACHA HALITAZIBIKA KAMWE. UTAKUMBUKWA DAIMA NA MKEO, WATOTO, WAJUKUU, NDUGU, MAJIRANI NA MARAFIKI ZAKO.

***RAHA YA MILELE UMPE EWE BWANA NA MWANGA WA MILELE AKUANGAZIE, UPUMZIKE KWA AMANI.***

HABARI KITAIFA

# Rais Magufuli atoa ahadi 10 wilayani Hai

**Na Gwamaka Alipipi,** HAI

MGOMBEA urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, ametoa ahadi ya kutatua kero sugu 10 katika Wilaya ya Hai, endapo atapata ridhaa ya kuongoza kwa miaka mingine mitano.

Akizungumza jana na wakazi wa Hai kwenye uwanja wa 'Half London', mjini hapa. Dk. Magufuli aliwaahidi wakazi wa wilaya hiyo kuwatatulia kero hizo, wakimchagua mgombea ubunge wa CCM, Saasisha Mafue.

Dk. Magufuli alisema wakazi wa Hai walijitakia wenyewe kuwa na matatizo yaliyobabishwa na aliyekuwa mbunge wao ambaye hakuwa anawasilisha bungeni matatizo yao.

"Mlinipa kazi ngumu, mtihani mkubwa, adhabu kali mlipomchagua mbunge wa upinzani kuongoza jimbo hili, mtu mwenyewewe hakuwa anahudhuria bungeni, alikuwa anatoka," alisema Dk. Magufuli na kuongeza: "Mwaka 2015 mlinipa kura na kuwa rais lakini mlininyima mbunge na madiwani, yaani ni sawa na kumfunga mtu mikono na miguu alafu unamwambia akuletee maji," alisema Dk.Magufuli.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Magufuli alisema Wilaya ya Hai inakabiliwa na kero nyingi ambazo zinahitaji kutatuliwa na mbunge wa CCM, ambaye ni Mafue.

**SOKO LA KISASA**

Dk. Magufuli alisema endapo wananchi wa Hai wakimchagua (yeye) pamoja na kumpitisha mbunge wa CCM, atahakikisha anawajengea soko la kisasa eneo la kwa Sadara, ambalo litakuwa linauza bidhaa kama vile ndizi.

**UMEME WA REA**

Vilevile, Dk. Magufuli aliwahakikishia baadhi ya wananchi katika vitongoji vya Hai kuwa atawaletea umeme wa Rea.

Dk. Magufuli alisema tatizo la ukosefu wa maji katika Wilaya ya Hai kumesababishwa na uchakavu wa miundombinu, hivyo katika kipindi cha miaka mitano ijayo, serikali itahakikisha inakarabati na kuleta maji katika eneo la Boma Ng'ombe.

"Najua maji ni shida Hai, lakini kama tumefanikiwa kutoa maji katika ziwa Victoria na kuyasambaza katika mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Tabora na Singida, kweli tushindwe kuwaletea maji Hai? Sasa nileteeni Mafue akasafishe hii kero. Matatizo ya Hai akayaweke katika utulivu," alisema Dk.Magufuli.

**KITUO CHA AFYA**

Kadhalika, Dk. Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo atahakikisha kunajengwa kituo cha afya katika eneo la Longoli.

Dk. Magufuli alisema tatizo la maslahi hafifu ya wafanyakazi katika mashamba na viwanda, atalishughulikia kwa kumtuma atakayekuwa mbunge wa jimbo hilo, Saashisha.

**BARABARA**

Rais Magufuli pia aliwaahidi wakazi wa Hai kuwajengea barabara ya Rongai yenye urefu wa kilometa 25, ambaye imekuwa kero kwa muda mrefu. "Tumejenga madaraja makubwa yanapita kwenye maji, tutashindwaje kujenga kilometa 25?, tumejenga mradi wa reli ya kisasa kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro, tumetoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu". Dk.Magufuli aliwaahidi wakazi wa Hai kuwaongezea watumishi wa afya 403 ambao watafanya kazi katika hospitali mbalimbali wilayani humo. Alisema wakazi wa Hai wamekuwa wakikabiliwa na kero ya kutokuwa na eneo la kutupa taka pamoja na magari ya kubebea takataka. Alisema endapo wakazi wa wilaya hiyo wakimchagua Saasisha kuwa mbunge wao, pamoja na kumpigia kura ya urais Dk. Magufuli atahakikisha kunatengwa eneo maalum la kutupia taka pamoja na magari ya kubebea.

**MGOGORO ARDHI**

Dk. Magufuli alisema kumekuwapo na mgogoro wa ardhi kwa miaka mingi kati ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) na wananchi wanaozunguka uwanja huo, wa maeneo ya Mtakuja, Sanya Station. Hivyo, aliwahakikisha wakazi wa maeneo yanayozunguka uwanja huo kuwatatulia mgogoro huo.

Kadhalika, Dk. Magufuli alisema kuna kiwanda cha 'Kilimanjaro Machine tools' ambacho kimekuwa kikiwakodisha wananchi mashamba kwa ajili ya kulima.Alisema serikali itahakikisha inatatua kero hiyo katika kipindi cha miaka mitano ijayo.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (kushoto), akimshukuru Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati Zanzibar, Salama Aboud Talib, baada ya kupokea zawadi katika hafla maalum ya mafanikio ya miaka 10 ya uongozi wake, iliyoandaliwa na wizara zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar walipomuaga rasmi katika viwanja vya Ikulu, mjini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Lissu aahidi Muungano wenye usawa

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA urais, Tundu Lissu (CHADEMA), amesema akiwa rais wa nchi, atahakikisha Muungano unazingatia usawa na maslahi ya pande zote mbili.

Lissu aliyasema hayo jana wakati Chama cha ACT-Wazalendo kilipokuwa kinafunga kampeni zake kisiwani Pemba, kikimwalika mgombea huyo wa urais wa Tanzania na Shekhe Ponda Issa.

Alipopewa nafasi ya kuhutubia, Lissu alisema anamuunga mkono Mgombea Urais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharrif Hamad (ACT-Wazalendo) kudai haki ya Wazanzibar ili kuwa na mamlaka yao baada ya uchaguzi.

Lissu alisema yeye na Maalim Seif wakiingia madarakani, watahakikisha wanaunda Muungano ulio bora kwa maslahi ya Watanzania wote.

"Hatuwezi kuendelea na Muungano ambao una sura ya kikoloni, kwa hivyo mimi nikiongoza Tanzania na Maalim Seif kuiongoza Zanzibar, tutaunda Muungano wenye maslahi na wananchi," aliahidi Lissu.

Lissu pia alitumia nafasi hiyo kuwahakikishi Wazanzibar kuwa yeye na chama chake wamekubaliana kuwa kwa Zanzibar watamuunga mkono Maalim Seif kwa nafasi ya urais.

Aliwaomba wapigakura wa Pemba kuwaunga mkono wagombea wote wa CHADEMA katika nafasi za ubunge na uwakilishi katika maeneo ambayo ACT-Wazalendo haina wagombea. "Ndugu zangu, adui yetu nambari moja ni CCM, kwangu mimi ACT siyo adui yangu. Kwa hiyo, tukae pamoja ili tuondoe CCM," alisema Lissu.

Katika mkutano huo, Maalim Seif pia alisisitiza uamuzi wao wa kumuunga mkono Lissu katika kinyang'anyiro cha urais wa Tanzania.

Alisema wameamuwa kumuunga mkono kutokana na uwezo wake na nia ya dhati ya kutetea mambo yenye mustabali na maslahi kwa Zanzibar.

Maalim Seif alisema akiingia madarakani, atahakikisha anaongoza nchi kwa misingi ya utawala bora, akiahidi kuifungua Zanzibar kiuchumi na kujenga bandari mbili kubwa katika visiwa vya Unguja na Pemba.

**KUKUBALI MATOKEO**

Katika hatua nyingine, Lissu amesema asiposhinda katika uchaguzi huru na wa haki, atakuwa wa kwanza kuutangazia umma kwamba ameshindwa. Alitoa msimamo huo jana alfajiri alipohojiwa na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) kuhusiana na mambo mbalimbali kuelekea uchaguzi mkuu.

Lissu amekuwa mgombea wa pili wa urais kutoa masharti ya kukubali matokeo ya uchaguzi baada ya juzi Maalim Seif kueleza kuwa atakubali matokeo ikiwa uchaguzi ukiwa huru na wa haki.

## Marekani yasema haiungi mkono chama chochote

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa Marekani nchini, Donald Wright, amesema Marekani haimuungi mkono mgombea au chama chochote cha siasa katika uchaguzi mkuu wa Tanzania.

Balozi Wright, ametoa kauli hiyo jana katika taarifa aliyoitoa kuhusu maoni yake ya uchaguzi mkuu nchini, unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28.

Alisema cha msingi Marekani katika uchaguzi huo ni kuona unakuwa huru, wa haki na wa kuaminika na kwamba matokeo yake yataakisi maamuzi ya watu wa Tanzania kama walivyoyaeleza katika sanduku la kura. "Hiki ndicho kielelezo halisi cha demokrasia," alisema Balozi Wright katika taarifa yake hiyo.

"Njia mojawapo ya kuhakikisha mchakato wa uchaguzi wenye uwazi ni kuruhusu waangalizi huru kushuhudia uchaguzi huo na kuwapa uhuru wa kueleza kile walichokishuhudia," alisisitiza.

Pia, alisema maofisa wa uchaguzi wanaweza kupiga hatua kubwa ya kurejesha imani ya watu kwa mchakato wa uchaguzi kwa kuhakikisha kuwa matokeo katika vituo vya kupigia kura yanawekwa wazi kwa umma.

Alisema kuhakikisha mawakala wote wa vyama wanaapishwa na katika siku ya uchaguzi wanaruhusiwa kuingia katika vituo vya kupigia na kuhesabia kura nchini kote pamoja na kupatiwa nakala za majumuisho ya kura mwishoni mwa zoezi la kuhesabu kura.

"Kama alivyosema Jaji wa Mahakama Kuu ya Marekani, Louis Brandeis, "mwanga wa jua ni dawa nzuri zaidi ya kuua vimelea vya maradhi (sunlight is the best disinfectant"). Kwa maneno mengine, uwazi wa serikali unaweza kuhakikisha kuwa mchakato wa uchaguzi unakuwa wa kuaminika."

Akizungumzia uhusiano kati ya Marekani na Tanzania, alisema unawarejesha siku za mwanzo za uhuru na urafiki kati ya Rais Kennedy na Mwalimu Nyerere ulioweka misingi ya ushirikiano imara uliojengwa katika kuheshimiana na kuelewana na kiini cha uhusiano huo kikiwa ni kuleta hali bora zaidi na ustawi wa watu wa nchi zote mbili.

Alisema mwaka 2020, Marekani itachangia zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 546 katika jitihada za maendeleo ya kiuchumi na kijamii za Tanzania. Aidha, katika kipindi cha zaidi ya miaka 20 iliyopita Marekani imetoa msaada wa zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni 7.5 kwa Tanzania, sehemu kubwa ya msaada huo ukielekezwa katika kuboresha afya ya Watanzania.

Alisema Serikali ya Marekani inawekeza kwa watu wa Tanzania kwa kuwawezesha vijana wake wenye vipaji mbalimbali kushiriki katika programu za mabadilishano ikiwamo ya kuwajengea uwezo wa kiuongozi vijana wa Afrika (Young African Leaders Initiative -YALI). Hali kadhalika, sekta binafsi ya Marekani imewekeza pia nchini Tanzania, ikichangia kuongeza nafasi za ajira kwa Watanzania na kukuza ustawi kwa nchi hizo mbili.

"Nikiwa nahimiza umuhimu wa biashara na uwekezaji, nimekuwa pia nikipaza sauti kuelezea umuhimu wa haki za msingi za binadamu na michakato ya kidemokrasia - ikiwa ni pamoja na uchaguzi huru na haki kama msingi muhimu sana wa maendeleo endelevu," alisema.

## HABARI MICHEZO

# GUTI AWAVUTA NEYMAR,MBAPPE REAL MADRID

**MADRID, Hispania**

GWIJI wa Real Madrid, Guti amesema angewasajili wakali wa Paris Saint-Germain, Neymar na Kylian Mbappe kwa Los Blancos hao, huku akiibeza Barcelona kwa usajili wa Antoine Griezmann.

Mabingwa hao wa LaLiga, Madrid wamekuwa wakihusishwa sana na mpango wa kuwania kumsajii Mbappe, ambaye mkataba wake na miamba hao wa jiji la Paris utamalizika mwishoni mwa msimu wa 2021-22.

Neymar, ambaye alisajiliwa kutoka Barcelona kwenda PSG kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222 mwaka 2017, awali alikuwa akihusishwa na Madrid.

Wakati Madrid wakijiandaa na mchezo wa El-Clasico dhidi ya wapinzani wao Barca utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Camp Nou, Guti aliwazungumzia Neymar na Mbappe huku akicheka usajili wa Griezmann, ambaye amekuwa na wakati mgumu wa kujiimarisha yeye mwenyewe tangu atue hapo akitokea Atletico Madrid mwaka jana.

"Ningemsajili Neymar na Kylian Mbappe kwa Real Madrid na Barcelona nisingemsajili yoyote, nashangaa kumsajili Griezmann," alisema Guti mwenye umri wa miaka 43, wakati akijadili kuhusu mchezo wa El-Clasico.

"Kuna wachezaji wengi wakubwa kwenye mchezo huu, lakini mimi napenda zaidi wachezaji vijana.

"Kwa uhakika ningekuwa na Ansu Fati pale Barcelona na Vinicius (Junior) kule Real Madrid (ambao wana mchango).

"Ni wachezaji wenye vipaji vya ukweli na ambao wataleta mambo mengi mazuri kwenye LaLiga."

## Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together we can build a better life)

### UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

#### WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2020

*(Kiasi kwa Shilingi Milioni )*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2020 | Robo Mwaka iliopita 30 Juni 2020 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| | 1 Fedha Taslimu | 642.86 | 868.48 |
| | 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 3,112.17 | 9,141.69 |
| | 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 31,962.94 | 27,017.89 |
| | 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,568.25 | 623.14 |
| | 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 35.29 | 108.86 |
| | 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 Bili zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 34,416.03 | 33,767.13 |
| | 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 44,648.55 | 36,268.16 |
| | 12 Mali Nyingine | 736.78 | 850.70 |
| | 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,241.33 | 1,350.25 |
| | **16 JUMLA YA MALI** | **118,364.20** | **109,996.28** |
| B | **DHIMA** | | |
| | 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 29,090.00 | 26,845.00 |
| | 18 Amana za Wateja | 49,640.92 | 44,206.80 |
| | 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | 20 Amana Maalumu | - | - |
| | 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| | 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| | 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,698.17 | 1,310.63 |
| | 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| | 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitaka | - | - |
| | 27 Dhima Nyingine | 607.83 | 673.95 |
| | 28 Madeni | - | - |
| | **29 JUMLA YA DHIMA** | **81,036.92** | **73,036.38** |
| | **30 MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29* | **37,327.28** | **36,959.90** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| | 32 Akiba ya Mtaji | 833.35 | 880.66 |
| | 33 Mapato Yaliyobakizwa | 2,303.93 | 2,256.62 |
| | 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,360.00 | 992.62 |
| | 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| | 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| | **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **37,327.28** | **36,959.90** |
| | 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 7,557.59 | 16,878.33 |
| | 39 Mikopo Chechefu | 4,218.70 | 4,219.68 |
| | 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 102.64 | 110.72 |
| | 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 31.54% | 33.60% |
| | (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 9.43% | 11.60% |
| | (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 56.82% | 51.18% |
| | (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 37.72% | 32.97% |
| | (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 95.13% | 88.80% |
| | (vi) Ongezeko la Amana | 10.81% | -0.11% |
| | (vii) Ongezeko la Mali | 7.61% | 0.38% |

#### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2020

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2020 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30 Septemba 2019 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Septemba 2020 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Septemba 2019 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 2,120.63 | 2,003.96 | 6,325.33 | 5,821.03 |
| 2 Gharama za Riba | 857.32 | 756.70 | 2,428.39 | 1,949.83 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,263.31** | **1,247.26** | **3,896.94** | **3,871.20** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (8.08) | 40.32 | (60.26) | 160.32 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba** | **110.07** | **137.28** | **449.57** | **632.91** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 39.25 | 19.30 | 135.49 | 105.98 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 70.82 | 117.98 | 314.08 | 526.93 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **864.09** | **947.18** | **2,536.78** | **3,054.38** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 317.93 | 436.87 | 963.69 | 1,201.20 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 8.11 | 6.20 | 17.46 | 19.32 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 538.04 | 504.11 | 1,555.63 | 1,833.86 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **517.38** | **397.04** | **1,870.00** | **1,289.41** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 150.00 | 160.00 | 510.00 | 440.00 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **367.38** | **237.04** | **1,360.00** | **849.41** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 25 | 23 | 25 | 23 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 11 | 7 | 41 | 26 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 11 | 7 | 41 | 26 |
| **14 Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.24% | 0.93% | 1.63% | 1.11% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 3.96% | 2.69% | 4.94% | 3.21% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 62.92% | 44.24% | 58.36% | 67.81% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 4.53% | 5.47% | 5.15% | 5.66% |

#### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2020

*(Kiasi kwa shilingi milioni )*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2020 | Robo Mwaka iliopita 30 Juni 2020 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Septemba 2020 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Septemba 2019 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 367.38 | 471.00 | 1,360.00 | 849.41 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| Hasara katika mali | 108.92 | 107.35 | 327.98 | 720.00 |
| -Badiliko halisi katika Mikopo | (8,380.40) | 2,253.04 | (9,014.54) | - |
| Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Amana | 7,679.13 | (79.50) | 8,831.46 | 1,099.47 |
| Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 529.79 | 234.96 | 863.35 | (62.20) |
| Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | (324.64) | (2,688.16) | (1,794.99) | 30.40 |
| Kodi iliyolipwa | (150.00) | (150.00) | (510.00) | - |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(169.82)** | **148.68** | **63.25** | **2,637.08** |
| **II Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za kudumu | 0.00 | (4.74) | (13.12) | (19.39) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | 5,285.43 | (15,011.15) | (4,114.55) | (6,776.56) |
| Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **5,285.43** | **(15,015.89)** | **(4,127.67)** | **(6,795.95)** |
| **III Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | (58.25) | (56.83) | (189.66) | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(58.25)** | **(56.83)** | **(189.66)** | **-** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 5,057.35 | (14,924.04) | (4,254.08) | (4,158.87) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 39,058.44 | 53,982.48 | 48,369.87 | 48,484.33 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **44,115.79** | **39,058.44** | **44,115.79** | **44,325.46** |

#### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2020

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 30/09/2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **2,308.69** | **828.58** | **-** | **-** | **35,967.28** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,360.00 | - | - | - | **1,360.00** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (4.77) | 4.77 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | **-** | **3,663.93** | **833.35** | **-** | **-** | **37,327.27** |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **1,125.67** | **45.93** | **493.37** | **-** | **34,494.97** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,472.31 | - | - | - | **1,472.31** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (782.65) | 782.65 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 493.37 | - | (493.37) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **2,308.69** | **828.58** | **-** | **-** | **35,967.28** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPETMBA 2020**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 20-10-2020 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 20-10-2020 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 20-10-2020 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| 1. RAJAB SELEMAN KAKUSA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 20-10-2020 |
| 2. INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 20-10-2020 |
| 3. MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 20-10-2020 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**



# SIMEONE: TUMEFUNGWA KICHAPO CHA FEDHEHA

**MUNICH, Ujerumani**

DIEGO Simeone amesema kichapo cha Atletico Madrid cha mabao 4-0 kutoka kwa Bayern Munich kimewaacha na "ladha mbaya" lakini alikataa kuwashutumu wachezaji wake.

Atletico walijikuta kwenye wakati mgumu katika mchezo huo wa Kundi A wa ufunguzi hatua ya makundi hapa mjini Munich, Jumatano huku winga wa Bayern, Kingsley Coman akionyesha mchango mkubwa katika matokeo hayo.

Nyota wa kimataifa wa Ufaransa, Coman alifunga mabao mawili - huku mengine mawili yakifungwa na Leon Goretzka na Corentin Tolisso kwa mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kichapo hicho kilikuwa kibaya zaidi kwa Atletico katika mashindano hayo ambayo waliweza kupiga shuti moja tu lililolenga goli, lakini Simeone aliachwa na mtazamo chanya kwa wachezaji wake.

"Nimeachwa na ladha mbaya kwa kipigo," alisema Simeone akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo. "Lakini nimeachwa na vitu ambavyo kwa uhakika tutavifanyia kazi na tutarudi kwenye kiwango chake.

"Sijui kama tulifanya makosa mengi au ulikuwa ubora wa wapinzani wetu, hivyo naondoka na mtizamo wa kuangalia nini cha kufanya na naamini mambo yatabadilika kwa siku sijazo."

# KLOPP ASIFIA KIWANGO CHA FABINHO

**AMSTERDAM, Uholanzi**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesifia kiwango cha Fabinho kwenye mchezo dhidi ya Ajax, huku akisisitiza hakushangazwa na kile kilichofanywa na nyota huyo wa Brazil.

Huku Virgil van Dijk akiwa nje ya dimba kutokana na majeruhi ya goti, Fabinho alianza kama mlinzi wa kati pamoja na Joe Gomez wakati Liverpool walipoanza mchezo wao wa kwanza wa makundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa ushindi wa bao 1-0, pale jijini Amsterdam, Jumatano.

Wote walionyesha kiwango cha kuvutia na Fabinho aliokoa hatari nne za wazi kuelekea langoni mwake.

Klopp aliridhishwa mno na kiwango cha mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil wakati Nicolas Tagliafico akijifunga kipindi cha kwanza na kuwawezesha Liverpool kuondoka na ushindi huo kwenye mchezo wa Kundi D.

"Huu ni muunganiko mzuri sana wa Joey na Fabinho, sidhani kama wameshawahi kucheza pamoja hapo kabla, sina uhakika kwa asilimia 100.

"Pengine mara moja, lakini kwa uhakika sijui," alisema akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

## HABARI MICHEZO

# FERNANDINHO KUKAA NJE WIKI SITA

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola anatarajia nahodha Fernandinho kuwa nje ya uwanja kati ya wiki nne hadi sita baada ya kiungo huyo kuumia wakati Manchester City ikipata ushindi dhidi ya Porto.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil ambaye aliingia dakika ya 85 kwenye mchezo huo wa Jumatano wa Kundi C pale katika dimba la Etihad, lakini alishindwa kumaliza mchezo baada ya kuumia mguu.

Aliumia mara kadhaa nyama za paja katika misimu ya hivi karibuni, na kushuhudia akikosa mechi 15 misimu miwili iliyopita wakati City iliposhinda mataji matatu.

Na Guardiola, ambaye alikuwa bila Gabriel Jesus, Nathan Ake, Benjamin Mendy, Kevin De Bruyne na Aymeric Laporte dhidi ya Porto, na sasa anatarajiwa kumkosa kiungo huyo.

“Ni habari mbaya. Ni sehemu ambayo aliumia awali,” alisema Guardiola akiiambia BT Sport. “Atakuwa nje kwa muda mrefu. Imetokea.”

Fernandinho amecheza mechi 228 kwenye Ligi Kuu England tangu alipojiunga na City mwaka 2013, mara kwa mara akitumika kama mlinzi wa kati.

# OZIL ATUMA UJUMBE WA SIMANZI ARSENAL

**LONDON, England**

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil amesema timu hiyo imemkatisha tamaa baada ya kuachwa kando katika majina 25 ya wachezaji watakaocheza Ligi Kuu ya England msimu huu.

Ozil mwenye umri wa miaka 32, ambaye alijiunga na timu hiyo mwaka 2013 kwa ada ya pauni milioni 42.4, hajacheza mechi ya ushindani ndani ya Arsenal tangu Machi, mwaka huu.

Pengine ni wakati mgumu zaidi kwake baada ya kuwekwa kando pia kwenye kikosi cha wachezaji 23 ambao wanatakiwa kucheza michuano ya Ligi ya Europa na mkataba wake unafikia tamati mwishoni mwa msimu 2021.

Baada ya kuachwa, Ozil kiungo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ujerumani na Real Madrid aliandika ujumbe wenye simanzi kwa mashabiki wa timu hiyo.

“Utu katika nyakati hizi hauthaminiki hata kidogo. Imeniumiza jina langu kutojumuishwa kwa wachezaji wa Arsenal watakaocheza Ligi Kuu England na mara zote nimekuwa nikifanyiwa visivyo hapa, lakini nilibakia katika mtazamo chanya wiki hadi wiki katika klabu ambayo naipenda zaidi, nitaendelea kujituma kwenye mazoezi labda naweza kurudishwa kwenye kikosi.”

Tangu alipojiunga na Arsenal akitokea Real Madrid miaka saba iliyopita, Ozil amefunga mabao 44 katika mechi 254 katika mashindano yote ndani ya kikosi hicho cha Washika Bunduki wa London.

# CONTE AKATAA KUWALAUMU WACHEZAJI

**MILAN, Italia**

ANTONIO Conte amesema hawezi kuwashutumu wachezaji wake wa Inter Milan licha ya kuhitaji bao la dakika ya 90 la kusawazisha kutoka kwa Romelu Lukaku na kupata sare ya 2-2 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Borussia Monchengladbach.

Inter walionekana wamejiandaa kupata ushindi wakati Lukaku alipofunga bao la kwanza mapema, lakini penalti ya Ramy Bensebaini na bao la Jonas Hofmann ilionekana kama miamba hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kuelekea kupata pointi tatu, juzi Jumatano.



Lukaku alifanya jitihada binafsi na kusawazisha bao dakika ya mwisho kwa Inter, ambao walimpoteza Alexis Sanchez aliyepata majeruhi kwenye mchezo huo wa Kundi B.

Na kocha wa Inter, Conte alikataa kuwalaumu wachezaji wake na alisema kumpoteza mlinzi wake wa pembeni, Achraf Hakimi kutokana na virusi vya corona kabla ya mchezo huo kulikuwa na athari kubwa kwao.

“Tunatakiwa kuangalia namna ya kuwa kwenye ubora wetu tukiwa uwanjani,” alisema Conte akiiambia Sky Sport Italia.

“Hicho ndio pekee tunachoweza kukifanya. Mambo hayakuwa rahisi leo (juzi), tulipata taarifa za Hakimi kuwa na corona saa chache kabla ya mchezo.

“Hadi asubuhi alikuwa anafanya mazoezi na kikosi na alitakiwa kuanza, hivyo nilijiandaa kumtumia, lakini kukosekana kwake kulikuwa na athari kubwa kwenye kikosi chetu.”


**Canara Bank (Tanzania) Ltd.**
*(Together we can build a better life)*

**DISCLOSURE UNDER REGULATION 12 OF BANKING & FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS 2014**

**CUSTOMER COMPLAINT REDRESSAL MECHANISM: To The Esteemed Customers Canara Bank (Tanzania) Ltd Tanzania**

**1. INTRODUCTION (UTANGULIZI)**

The Complaints Resolution Desk (the Desk) has been established by the Bank of Tanzania (BOT) as a cost effective and efficient mechanism to resolve complaints between banking institutions and their customers. The Desk, which is fully funded by the Bank, is intended to resolve complaints (small claims) whose monetary value in respect of both the claim amount and remedy awarded does not exceed fifteen million Tanzania shillings (15,000,000) Mn.

**2. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH OUR BANK (JINSI YA KUWASILISHA MALALAMIKO KWA DAWATI)**

When you are dissatisfied with our services or you have any complaint pertaining to our staff or bank or otherwise, you may lodge complaint to us in writing by post or fax or through your registered email address on the following contact addresses.

**General Manager (Operations) Canara Bank (Tanzania) Ltd,**
**Dar es Salaam Branch,**
**Post Box 491 Dar es Salaam**
**Phone : +255 (22) 2112532**
**Fax: +255 (22)2112534**
**E Mail : cbtl@canarabank.co.tz**

**The Nodal Officer, Grievance Redressal Cell,**
**Canara Bank (Tanzania) Ltd**
**Post Box 491 Dar es Salaam,**
**Phone : +255 (22) 2112530;**
**Fax: +255 (22)2112534**
**E Mail compliance.cbtl@canarabank.co.tz**

**NOTE:**
- For lodging complaint with BOT please use Complaint Form No 1.
- For detailed information for lodging compliant with BOT please visit BOT website https://www.bot-tz.org.

**3. INTERNAL COMPLIANT RESLUTION MECHANISM (MCHAKATO WA KUTAFUTA UFUMBUZI WA MALALAMIKO)**

We through our internal complaint handling mechanism shall resolve your complaints within 21 working days from the date of lodging the compliant. The Internal Complaint handling mechanism in our Bank is as under:
- Receiving and timely processing consumers' complaints.
- Keeping complainants updated throughout the process.
- Keeping a record of all complaints and submit it to the Bank of Tanzania on quarterly basis.
- Resolving all consumer complaints within 21 working days from the date of lodging the complaint.
- In exceptional circumstances if we are unable to resolve the complaint within 21 working days, we will immediately inform the complainant of our inability and reason for the inability and what measures are being taken to resolve the matter urgently and in any case not more than 14 working days thereafter.

**4. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH THE DESK AT BANK OF TANZANIA (BOT) (NAMNA YA KUWASILISHA LALAMIKO KWA DAWATI LA BOT)**

If you are dissatisfied with the decision of our Bank in respect of your compliant or do not receive a response from our Bank within 21 working days from the date of lodging your complaint, you may within 14 working days lodge your complaint with the Desk at BOT. However, before lodging your complaint with the Desk at BOT, you are required to exhaust the Internal Complaints resolution mechanism of our Bank first.

The compliant with Complaints Resolution Desk at Bank of Tanzania shall be lodged in the prescribed form (Schedule A), duly signed by the complainant and shall be submitted in any of the following ways:

a) By hand or by post to:
Complaint Resolution Desk
Office of the Secretary to the Bank of Tanzania,
10 Mirambo Street,
11884, Dar es Salaam.

b) By electronic mail: complaints-desk@bot.go.tz
d) By facsimile to fax no: +255 22 2234067
e) By phone: +255 22 2233265/ +255 22 2233246

**Note:**
a) Complaints shall be lodged with the Desk from 9.00 AM to 12.30 Pm (Monday to Friday).
b) Your complaint must be lodged before expiry of two years after the cause of action arose.

**5. PECUNIARY JURISDICTION OF THE BOT DESK (MAMLAKA ZA KIFEDHA ZA DAWATI)**

The desk shall handle complaints whose total monetary value in respect of both the claim amount and remedy to be awarded does not exceed Fifteen Million Tanzania Shillings (TZS 15,000,000/-).

**6. ELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YA HAKI)**

Only the following categories of complaints are eligible for submission to the Desk;
a) A complaint against a banking institution which is either a member of the Tanzania Bankers Association or regulated by the Bank.
b) A complaint which is lodged within 14 days after a banking institution has delivered its decision or has failed to respond.
c) A complaint in respect of an incident which occurred less than two (2) years ago.

**7. INELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YASIYO NA HAKI)**

In terms of the Guidelines issued, the Desk considers the following complaints as ineligible:
a) A complaint which has been the subject of legal proceedings before a Court or Tribunal.
b) Where the complainant has not suffered any financial loss, material inconvenience or distress.
c) A complaint which would be more suitably dealt with by a Court or under other dispute resolution arrangement.
d) A complaint whose resolution would prejudice the rights of other parties who have not consented to the resolution by the Desk.
e) A complaint which is vexatious or frivolous or not in good faith.
f) A complaint which was not first reported to the banking institution concerned.
g) A complaint which is lodged more than 14 days after a banking institution has delivered its decision or failed to resolve the complaint.
h) A complaint which is beyond the pecuniary jurisdiction of the Desk.

**8. INFORMATION YOU MUST INCLUDE IN THE COMPLAINT (TAARIFA MUHIMU ZA KUJUMUISHA KWENYE LALAMIKO)**

a) Your name and address.
b) The name and address of the banking institution against which the complaint is made.
c) Details of what your complaint is about including exactly what the bank did that it shouldn't have done or what it didn't do that it should have done.
d) What you have lost in terms of personal injustice, financial loss, hardship or inconvenience.
e) What you would like the Desk to do to put things right and details of what you have done so far to try to resolve the complaint
f) Include documentary evidence, if any.

**9. WITHDRAWAL OF THE COMPLAINT (KUFUTA LALAMIKO)**

A complainant may, at any time before the Desk's determination, withdraw his complaint in writing from the Desk, and the matter shall be closed by the Desk.

**10. FREE SERVICE (HUDUMA ZA BURE)**

Resolution of banking consumers' complaints is free of charge as the Desk does not charge any fee whatsoever.

**11. MEDIUM OF COMMUNICATION (NJIA YA MAWASILIANO)**

The medium of communication is both English and Kiswahili.

**12. REMEDIES AWARDED (SULUHISHO LILILOPATIKANA)**

The function performed by the Desk is different from that performed by courts. The Desk is enjoined not to have regard to technicality and legal form but resolve complaints using criteria that would not usually be used by courts; for instance whether an explanation for the conduct was not given when it should have been given. A banking institution may be required to issue an apology, change its practices, effect payment or compensation as the case may be. The Desk is not bound by the legal principles of handling complaints such as rules of evidence but adheres to the general principles of natural justice.

When Aggrieved by Desk decision

Either party may request the Desk to reconsider any of its decision. Each party also has a right to seek redress before a competent court when it is not satisfied with the decision given by the Desk

**CANARA BANK (TANZANIA) LIMITED**
**SERVICES CHARG**

| | TZS | USD | D. REMITTANCES | | |
|---|---|---|---|---|---|
| A. SAVINGS BANK | | | | TZS | USD |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE | 1. TISS | 11,800.00 | $11.8 |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE | 2. E Remittances | | |
| 3. A/C Statement Charges | | | Upto USD 1000 or Eq. TZS | 20,000.00 | $10 |
| a) Monthly | FREE | FREE | 1001 to 5000 | 24,000.00 | $12 |
| b) Interm | 5,000.00 | $5 | 5001 to 10000 | 48,000.00 | $25 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | FREE | Upto 5000 Free Above 5000 - 0.3% | 10,001 and above | 100,000.00 | $50 |
| 5. Cash Deposit Charges | FREE | FREE | 3. SWIFT | | |
| 6. Balance Confirmation certificate | 15,000.00 | $7 | a) Swift Outward | | |
| 7. A/c Closure charges | 15,000.00 | $15 | Upto 5,000 | NA | $45 |
| 8. Activation of Dormat A/c | 6,000.00 | $6 | 5,001 to 10,000 | NA | $60 |
| B. CURRENT ACCOUNT | | | above 10,000 | NA | $90 |
| | | | b) Swift Inward | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE | Upto 5,000 | NA | $12 |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE | 5,001 to 10,000 | NA | $18 |
| 3. A/C Statement Charges a) Monthly b) Interm | 5000 5000+500 for each page | $5 $ 5+1 for each page | above 10,000 | NA | $30 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MIO- FREE ABOVE 25 MIO--0.12% | Upto 5000 Free 5000 to 10,000 - 0.3% Above 10,000 - 0.5% | E. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES | | |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO- FREE ABOVE 50 MIO--0.12% | Upto 10,000- Free > 10,000- 0.3% | 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - 25,000 5Mio to 10 Mio - 200,000 10 Mio to 25mio - 400,000 25 mn to 500 mio - 1.5% >500mio--1.25%* *minimum 7.5mio | Upto 5,000 - $100 5000 to 10,000 - $200 Upto 20,000 - $300 20,000 to 500,000 - 1.5% >500,000--1.25%* *minimum 7,500 |
| 5. Balance Confirmation certificate | 25,000.00 | $15 | 2. Documentation Charges | Upto 100 mio --NIL-- >100 Mio 0.3% -Min 300,000 | Upto 50,000 --NIL-- >50,000 - 0.3% Min 150 |
| 6. Stop Payment Charges | 30,000.00 | $15 | 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - 25,000 5 Mio to 10 Mio - 200,000 10Mio 25mio - 450,000 25 mn to 500 mio -1.8% >500mio--1.5%* *minimum 9mio | Upto 20,000 - $300 20,000 to 500,000 - 1.8% >500,000--1.5%* *minimum 9000 |
| 7. Cheque Return Charges | | | 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio -25,000 >100 mio - 50,000 | Upto 50,000 - 25 >50,000 ----50 |
| a) Inward | 30,000.00 | $15 | F. LETTER OF CREDIT | | |
| b) Outward | 30,000.00 | $20 | Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof) | | |
| 8. A/c closure charges | 25,000.00 | $20 | Opening commission | NA | 1.2% ( Min $ 200) |

| C. MOBILE BANKING CHARGES | | | LC amendment Commission | NA | 0.4% ( Min $50 max 350) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. Cash Withdrawal | | | Swift charge for LC opening | NA | $40 |
| Upto 100,000 | 2,000.00 | NA | Swift charge for other message/amendments | NA | $40 |
| 101,000 to 200,000 | 3,000.00 | NA | Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Min $200) |
| 201,000 to 400,000 | 5,000.00 | NA | LC cancellation charges | NA | 1.2% ( Min $200) |
| 401,000 to 600,000 | 6,000.00 | NA | Non payment of Bills on due date | NA | 16% Till Payment |
| 601,000 to 999,000 | 8,000.00 | NA | Export Letters of Credit (per quarter or part thereof) | | |
| 2. Funds Transfer/Mobile Wallet | | | Advising commission | NA | $140 |
| Upto 100,000 | 500.00 | NA | Confirmation Commission | NA | 0.5% ( Min $150) |
| 101,000 to 250,000 | 1,000.00 | NA | Negotiating bills under LC | NA | 0.5%(Min $75+cuourier+int) |
| 251,000 to 500,000 | 2,000.00 | NA | Reimbursement claim paid | NA | 0.5% ( Min$75) |
| 501,000 to 1,000,000 | 5,000.00 | NA | Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Min $200) |
| 1,001,000 TO 10 Mn | 10,000.00 | NA | Collection of Export LC | NA | 0.5%(Min $75+cuourier+int) |
| | | | Amendments | NA | $75 |
| Mobile Banking Services | | | G. Guarantees (Local & International) | | |
| A) Monthly Subscription Charges | 500.00 | NA | Bonds & Guarantees | 1.2% ( Min TZS 75,000) | 1.20% |
| B) PIN Request | 2,500.00 | NA | Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | 0.5% per quarter (Min TZS 75,000) | 40% of actual charges |
| H. LOCKERS RENT YEARLY | | | | | |
| 1.SMALL | 350,000.00 | | | | |
| 2. MEDIUM | 600,000.00 | | | | |
| 3. BIG | 750,000.00 | | | | |

| OTHER DISCLOSURES(VIAMBATANISHI) | | |
|---|---|---|
| | TZS | USD |
| 1. Base or Prime Lending Rate | 16 | 7 |
| 2. Maximum spread above Base or Prime Lending Rate | 4 | 4 |
| 3.Penal Interest | | |
| a. For non compliance on Terms of Saction | 3% p.a over regular rate of interest | |
| b. For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | 5% p.a over regular rate of interest | |
| 4. Deposit Rates | | |
| a. Current account | Nill | Nill |
| b. Savings bank deposit | 2.50% | 0.50% |
| c. Fixed deposits | | |

i. Fixed Deposits of TZS

| Amount in TZS | up to TZS 10 Million | TZS 10 to 100 Million | Above TZS 100 Million |
|---|---|---|---|
| 31-90days | 3.50% | 4.50% | 5% |
| 91-180days | 4.50% | 5% | 5% |
| 181-364 days | 6% | 6.50% | 6.50% |
| 1-2years | 7% | 7.50% | 8% |
| Over 2 years | 8% | 8.50% | 9% |

ii. Fixed Deposits of USD

| Amount in USD | up to USD 5000 | USD 5000-50,000 | Over USD 50,000 |
|---|---|---|---|
| 31-90days | 0.50% | 1% | 1.50% |
| 91-180days | 1% | 2% | 2.25% |
| 181-364 days | 2% | 2.25% | 2.75% |
| 1-2years | 2.25% | 2.75% | 3% |
| Over 2 years | 2.50% | 3% | 3.50% |

215819802

**Banking Services offered BY Canara Bank (Tanzania) Ltd** **We offer following Services**

- Current and Saving Account
- Salary Account
- Student Account
- Fixed Deposit Account
- Re Investment Deposit Account
- Recurring Deposit Account
- Overdraft and Term Loans
- Vehicle Loan
- Mortgage Loan
- Personal Loan
- Insurance Premium Funding
- Safe Deposit Lockers
- All Export and Import Related transactions
- Letter of Credit and Guarantees
- E- Remit Facility to India
- Mobile Banking




Plot No 16/1, Elia Complex
Zanaki-Bibi Titi Street, P.O.Box 491- Dar es Salaam, Tanzania
T: +255 222 112 2530 (D) +255 222 112 532
Email: cbtl@canarabank.co.tz

**Access your A/c 24x7**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ZIDANE AAHIDI KUMALIZA TATIZO LA UBORA MADRID

Afunguka tayari amepata 'dawa' ya kumaliza tatizo hilo huku akijiandaa kuwakabili Barca kesho...

**MADRID, Hispania**

ZINEDINE Zidane anaamini anaweza kuirudisha Real Madrid kwenye kiwango chake baada ya kukumbana na kichapo kwenye mchezo wa kwanza wa makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kutoka kwa Shakhtar Donetsk, juzi Jumatano.

Madrid hicho ni kipigo cha pili mfululizo katika mashindano yote chini ya Zidane ikiwa ni kwa mara ya kwanza, huku wakitoka kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya timu mpya iliyopanda daraja, Cadiz kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wikendi iliyopita.

Shakhtar ilikuwa inaongoza kwa mabao 3-0 kipindi cha kwanza wakati Madrid waliporuhusu nyavu zao kutikiswa mara tatu, ikiwa ni kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 15, kabla ya Los Blancos kupata mabao mawili kupitia kwa Luka Modric na Vinicius Junior.

Lakini mabao hayo hayakutosha kuwasaidia Madrid kuibuka na ushindi kwenye mchezo huo wa Kundi B.

Presha kubwa sasa kwa Zidane ipo kuelekea kwenye mchezo wa Jumamosi wa El Clasico dhidi ya Barcelona, lakini Zidane amebainisha kwamba anaamini kiwango cha timu hiyo kitarudi.

"Najiona mwenyewe kuwa na uwezo wa kumaliza tatizo hili, ndicho ambacho ninakwenda kukifanya," amesema Zidane, ambaye aliondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 msimu wa 2019-20.

"Naamini wachezaji watakwenda kujaribu na wana uwezo wa kubadilika na kupata matokeo tofauti kwa mechi zinazokuja.

"Tunakwenda kuangalia suluhisho ya kumaliza kabisa tatizo la kiwango kwa timu yetu na naamini tutapata.

"Kwa sasa tunajiandaa kwa ajili ya mchezo wa ugenini wa Jumamosi dhidi ya Barcelona ambao utakuwa mgumu kwa upande wetu."

Fowadi ambaye hayupo kwenye kiwango chake, Luka Jovic alianza na akatolewa dakika ya 59 na nafasi yake kuchukuliwa na Vinicius - ambaye aliongoza mashambulizi, huku Karim Benzema akiwa benchi na Eder Militao alikuwa 'patina' wa Raphael Varane kwenye safu ya ulinzi kutokana na kukosekana kwa nahodha Sergio Ramos.

## KWA UFUPI

**WHITE ANUKIA LIVERPOOL**

KLABU ya Brighton inaonekana itataka kiasi cha pauni milioni 50 ili kumwachia mlinzi wake wa kati, Ben White kama Liverpool watatafuta mtu wa kiziba pengo la Virgil van Dijk mwenye umri wa miaka 29, na kumsajili Mwingereza huyo mwenye umri wa miaka 23 kipindi cha dirisha dogo la usajili la Januari. ***(Sun)***

**MBAPPE KUONDOKA PSG**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe (21), anaweza kuondoka Paris St-Germain na kujiunga na Liverpool au Real Madrid kipindi kijacho cha majira ya joto. ***(Le Parisien)***

**GREENWOOD, UNITED WATETA**

WINGA wa Timu ya Taifa ya England, Mason Greenwood ambaye ana umri wa miaka 19, amezungumza na Manchester United kuhusu muda wa kucheza mara kwa mara. ***(Mail)***

**KEPA ANUKIA SEVILLA**

CHELSEA ipo tayari kumwachia golikipa wake, Kepa Arrizabalaga kuondoka Januari kwa mkopo, huku Sevilla ikifikiria kumchukua raia huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 26. ***(Estadio Deportivo)***

**OZIL AFUNGUKA**

KIUNGO wa Ujerumani, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 32, anaamini ofa ya matangazo ya biashara nchini China ya Arsenal ndio ilichangia yeye kuachwa kwenye kikosi cha Ligi Kuu na Ligi ya Europa. ***(Mail)***

**ROSE SAFARI IMEIVA**

KLABU ya Tottenham Hotspur inapanga kumwachia moja kwa moja mlinzi wake wa kushoto, Danny Rose mwenye umri wa miaka 3. ***(Football Insider)***

**WELBECK AIKATAA FENERBAHCE**

MSHAMBULIAJI wa England, Danny Welbeck (29), amekataa ofa ya kulipwa mshahara wa pauni 140,000 kwa wiki ili akajiunge na klabu ya Ligi Kuu Uturuki, Fenerbahce - na kuamua kubakia Ligi Kuu England pale Brighton. ***(Sun)***

**ZAKARIA AGOMBEWA ENGLAND**

CHELSEA inawania saini ya kiungo wa Borussia Monchengladbach, Denis Zakaria mwenye umri wa miaka 23, lakini inakabiliwa na ushindani kutoka Manchester United na Manchester City kwa nyota huyo wa kimataifa wa Uswisi. ***(Bild via Express)***

**SHEFFIELD YAMTAKA SWIFT**

KLABU ya Sheffield United ipo tayari kufufua mpango wake wa kumwania kiungo wa Reading, John Swift ambaye ana umri wa miaka 25. ***(Sheffield Star)***

**DEENEY KUONDOKA WATFORD**

NAHODHA wa Watford, Troy Deeney mwenye umri wa miaka 32, amesisitiza hayupo tayari kuwa chaguo la pili klabuni hapo, huku akiwaniwa na Tottenham na klabu nyingine za Ligi Kuu Englamd. ***(Talksport)***

**FERNANDES KURUDI BENFICA**

KIUNGO wa Ureno, Gedson Fernandes mwenye umri wa miaka 21, anayecheza kwa mkopo Tottenham anaweza kurudi katika klabu yake ya zamani ya Benfica wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari. ***(RTP 3, via Sun)***

**TORREIRA: SIRUDI ARSENAL**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Lucas Torreira mwenye umri wa miaka 24, hana mpango wa kurudi Arsenal na anataka uhamisho wake wa mkopo pale Atletico Madrid kuwa wa kudumu. ***(Ovacion Digital, via Star)***

## HABARI MICHEZO

# KMC YATANGULIA MWANZA KUISUBIRI YANGA JUMAPILI

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha KMC FC kiliwasili salama mapema jijini Mwanza jana mchana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Habib Kondo amesema hataki kuona wanapoteza mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kondo alisema licha ya 'kudondosha' pointi katika mechi mbili zilizopita, lakini wachezaji wake hawakuonyesha kiwango kibaya na hivyo wanaendelea kujiimarisha ili kutimiza malengo yao.

Kondo alisema kila mchezaji ameahidi kuonyesha kiwango kizuri kwa sababu wanataka kuona wanaifunga Yanga na kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 18.

Alisema tayari ameyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi zilizopita ambazo walizopoteza na hawatarudia makosa waliyofanya kwa lengo la kuwapa furaha mashabiki wao.

"Tumejipanga vizuri, tufanya vizuri katika mechi zijazo, sasa tunaendelea na maandalizi yetu kwa ajili ya kuwakabili Yanga, tunataka kuhakikisha tunapata ushindi na si matokeo mengine katika mechi hiyo."

"Tunawaheshimu Yanga, ni timu iliyofanya usajili mzuri, hata na sisi pia tuko vizuri kwa ajili ya kupata matokeo, bila ya kuangalia majina ya wapinzani wetu tunaocheza nao," Kondo alisema.

Ofisa Uhusiano wa timu hiyo, Christina Mwagala, aliliambia gazeti hili kikosi cha KMC kilitarajia kufanya mazoezi jana na kila mchezaji aliyekwenda Mwanza yuko kwenye hali nzuri.

Mwagala alisema KMC imejiandaa kufanya vyema katika mechi zao tatu zinazofuata na wanaamini hilo linawezekana kama walivyoanza msimu huu kwa ushindi.

"Tuna mechi dhidi ya Yanga, halafu tutabakia Mwanza kwa ajili ya kucheza na Gwambina Oktoba 30, mwaka huu na baadaye tutawafuata Biashara kwenye Uwanja wa Karume ulioko mkoani Mara," alisema Mwagala.

KMC ndio mwenyeji wa mechi hiyo na imeuchagua Uwanja wa CCM Kirumba kwa kufuata kanuni ya ligi inayoruhusu timu kutumia uwanja mwingine tofauti katika mechi zake mbili.




Mwanasheria wa timu ya Lipuli, Jackson Chaula (mwenye tai), akibadilishana mkataba wa udhamini na Meneja wa Kampuni ya VunjaBei, Fadhili Ngajilo (kushoto), uliosainiwa mkoani Iringa jana. Kampuni hiyo itakuwa inaipatia Lipuli inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza vifaa mbalimbali vya mazoezi kwa muda wa mwaka mmoja. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Azam yataja siri ya ushindi

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushinda mechi zake saba mfululizo, uongozi wa Azam FC umesema siri ya mafanikio yao msimu huu ni kuimarika kwa ushirikiano kati ya wachezaji, benchi la ufundi na usajili mzuri waliofanya msimu huu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema lengo la timu hiyo msimu huu ni kushinda kila mechi na hatimaye kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Popat alisema wamejipanga kupata matokeo chanya katika kila mechi na hawatajali watakuwa wanacheza na timu ipi na wakati gani.

"Kikubwa ni mikakati na sisi kuwa pamoja na benchi la ufundi na wachezaji. Awali mshikamano ulikuwapo, lakini safari hii tumeuzidisha, wachezaji wanajituma, na hata wachezaji tuliowaongeza ni wazuri, lakini pia wamepata muunganiko haraka na wenzao, ndiyo maana unaona timu imekuwa hivyo," alisema Popat.

Kuhusu mechi zao dhidi ya Simba na Yanga, alisema wadau wamekuwa wakimuuliza kama timu yake inaweza kuzifunga timu hizo, lakini anavyofahamu ligi ina mechi 34 ambazo zinatakiwa kuchezwa na kufanya vizuri.

"Siangalii kumfunga Simba au Yanga, hizo ni mechi nne tu, matokeo yoyote ambayo yatapatikana haijalishi, kinachotakiwa sisi Azam kushinda mechi 30 zilizobaki tutakuwa mbali sana," Popat alisema.

Azam imeshinda mechi saba mfululizo za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu na kuvunja rekodi yake yenyewe iliyoiweka msimu wa 2015/16 iliposhinda mechi tano mfululizo kabla ya kutoka sare ya bao 1-1 kwenye mechi ya sita dhidi ya Yanga Oktoba 17, mwaka 2015.

Azam itashuka dimbani tena Jumatatu kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro kucheza dhidi ya Mtibwa Sugar.

## KVZ, JKU kamili kuwania ubingwa

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya KVZ na JKU ndiyo zimethibitisha kushiriki katika mashindano ya netiboli ya Ligi ya Muungano ambayo yatafanyika kuanzia Novemba 28, mwaka huu jijini Tanga imeelezwa.

Katibu Mkuu wa Chama cha Netiboli Zanzibar (Chaneza), Said Mansabu, alisema idadi hiyo ya timu ni ndogo na wanazikumbusha klabu nyingine kuthibitisha ushiriki wao.

Mansabu alisema wanahitaji kuona timu zinaongezeka katika kushiriki michuano hiyo ambayo itasaidia kupata mwakilishi bora wa nchi kwenye mashindano ya kimataifa.

Alisema licha ya kusuasua kwa mchakato wa awali, wanaamini mashindano hayo yatakuwa magumu na yenye ushindani kwa sababu kila timu huhitaji kutwaa ubingwa.

"Ninaomba timu nyingine ziendelee kujitokeza kuthibitisha kushiriki mashindano haya ya Ligi ya Muungano, ni michuano yenye kutoa nafasi kwa wachezaji kujiimarisha zaidi," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza bado wamekuwa wakiuendesha mchezo huo katika mazingira magumu kwa sababu ya kukosa taasisi na kampuni za kuwadhamini.

"Kwa upande wa Zanzibar mchezo huu hauna mwamko mkubwa kutokana na kukosa wafadhili, tunawaomba wadau mbalimbali wajitokeze kutuunga mkono," alisema Mnsabu.

## African Lyon yaipania Gipco

**Na Adam Nyangasa, TUDARCo**

KOCHA Mkuu wa African Lyon, Nizar Khalfan, amesema kikosi chake kimejipanga kuhakikisha kinapata ushindi katika mechi ya Ligi Daraja la Kwanza dhidi ya Gipco FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya.

Nizar aliliambia gazeti hili wachezaji wake wameendelea kufanya mazoezi vizuri na anaamini wataonyesha kiwango cha juu katika mchezo huo.

Kocha huyo alisema amefurahi kuona wachezaji wote wameimarika na wako tayari kukabiliana na ushindani watakaokutana nao kutoka kwa wenyeji wa mechi hiyo. "Napenda kuelezea kwamba maandalizi ya kikosi changu kuelekea mechi dhidi ya Gipco ni mazuri, 'fitnesi' ya wachezaji inaimarika kila siku wanavyoendelea kujinoa.

Alisema kwa sasa safu yake ya ulinzi imeimarika baada ya kuyafanyia kazi makosa yaliyoonekana kwenye mechi iliyopita na anaamini hawataruhusu tena vyavu zao kutingishwa kirahisi.

"Mchezo uliopita ulikuwa na makosa mengi na nimejaribu kuyafanyia kazi, kwa upande wa ulinzi timu iko vizuri ila kwenye ushambuliaji bado kuna matatizo madogo madogo, ukiangalia mchezo uliopita timu ilitengeneza nafasi nyingi, lakini umakini katika umaliziaji ulikua ni mdogo sana," alisema Nizar.

Aliongeza mechi za kirafiki ambazo timu yake ilicheza iliwasaidia kuimarisha muunganiko katika kikosi hicho ingawa aliwatupia lawama waamuzi wanaochezesha ligi hiyo.

Michezo
Ijumaa Oktoba 23, 2020
Nipashe



ZIDANE AAHIDI KUMALIZA TATIZO LA UBORA MADRID HABARI UK 22

# YANGA CHEREKO, SIMBA YATEPETA

Mrundi Kaze aanza vyema Ligi Kuu Bara huku Simba ikipoteza mechi ya kwanza...

**Na Adam Fungamwango**

YANGA imemkaribisha vyema Kocha Mkuu mpya, Cedric Kaze baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania wakati mabingwa watetezi, Simba, wakikubali kichapo cha goli 1-0 kutoka kwa 'Maafande' wa Prisons katika mechi za Ligi Kuu Bara zilizochezwa kwenye viwanja viwili tofauti nchini jana.

Matokeo hayo yameifanya Yanga kufikisha pointi 16 na kusogea hadi nafasi ya pili iliyokaliwa na watani zao Simba, ambao sasa wako katika nafasi ya tatu, wakibakia na pointi zao 13 na Prisons kufikisha pointi tisa na kupaa hadi nafasi ya nane kwenye msimamo.

Azam FC ambayo imecheza mechi saba, moja zaidi ya vigogo hao wa soka nchini, ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 21 huku Mbeya City yenye pointi mbili, ikiendelea kuburuza mkia.

Kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa Uhuru, iliwachukua Yanga dakika 21 kufanya shambulizi kwenye lango la Polisi Tanzania, baada ya Feisal Salum kuachia kombora kali lililopanguliwa na golikipa Peter Manyika na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Dakika tano baadaye, Fei Toto tena alifanya jaribio kama la mwanzo kwa kuachia shuti kali, lakini Manyika alikuwa makini na kuupangua mpira huo.

Kama si uhodari wa kipa huyo wa zamani wa Simba, huenda Yanga ingevuna magoli mengi kutokana na makosa mengi ya mabeki wa Polisi Tanzania wakiongozwa na Pato Ngonyani na Idd Mobby.

Bao pekee la Yanga lilifungwa dakika ya 69 na Mkongomani Tonombe Mukoko, baada ya mabeki wa Polisi Tanzania kusahau kumkaba na kuupata mpira ndani ya eneo la hatari akiwa hajakabwa, kabla ya kuachia shuti lililombabatiza mmoja wa mabeki wa timu hiyo na kumpoteza maboya Manyika na hatimaye kujaa wavuni.

Kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Mjini Sumbawanga, Simba ilipoteza mechi yake ya kwanza msimu huu dhidi ya Prisons kwa bao 1-0.

Bao hilo pekee katika mchezo huo lilifungwa na Samson Mbangula dakika ya 48, ambaye aliruka juu kuwazidi mabeki wa Simba na kupiga kichwa kilichotinga wavuni moja kwa moja, akimalizia krosi ya Michael Ismail.

Ulikuwa pia ni uzembe wa kipa wa Simba, Aishi Manula ambaye alikuwa ametoka golini, lakini kabla hajaufikia mpira alibadilisha uamuzi na kurejea katika nafasi yake, lakini alikuwa ameshachelewa kuuwahi mpira na hatimaye wenyeji kujipatia bao lililowapa pointi tatu.

Simba ambayo ilicheza bila wachezaji wake tegemeo hasa Claotus Chama, Meddie Kagere, John Bocco, Chriss Mugalu, haikuwa na uwezo wa kuipenya ngome ya Prisons, iliyoongozwa na Vedatus Mwihambi, Nurdin Chona, Benjamin Asukile, na Jumanne El Fadhili.

Prisons ilionekana kutumia zaidi mpira wa nguvu, pamoja na kukaa zaidi nyuma ya mpira kulinda na kushambulia kwa kushtukiza, ikitumia mipira mirefu.

Yanga itashuka tena dimbani Jumapili kuwavaa KMC katika mechi itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza wakati Jumatatu Simba itavaana na Ruvu Shooting huku Mtibwa Sugar wakiikaribisha Azam FC kwenye Uwanja wa Jamhuri, mkoani Morogoro.





Golikipa wa Polisi Tanzania, Peter Manyika (kulia), akiruka kudaka mpira katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Yanga iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. Yanga ilishinda 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## AZAM YATANGAZA KUSAKA POINTI 90

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC umesema akili na mawazo yao yako kwenye kutafuta pointi 90 ili kuutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na si kuwafikiria vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga.

Azam yenye pointi 21, baada ya kushinda mechi zote saba walizocheza, ndio wanaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema kwa msimu mmoja wanakutana na vigogo hao katika mechi nne, lakini wana michezo mingine muhimu 30 wanayohitaji kushinda ili kufikia malengo.

Popat alisema wanachopigania sasa ni kutafuta pointi tatu katika michezo hiyo isiyohusisha vigogo hao ili malengo waliyonayo yatimie.

**"Mechi za Simba na Yanga ni nne tu, ambazo ni sawa na pointi 12, tunaangalia zaidi pointi nyingi katika mechi 30, kila mechi kwetu tunaichukulia ni muhimu bila kujali tunakutana na timu gani," alisema Popat.**

Kiongozi huyo alisema mshikamano uliopo ndani ya klabu na usajili imara walioufanya umesaidia kuwapa matokeo mazuri katika michezo saba waliocheza.

"Msimu huu tunajambo letu, na kwa kuwaheshimu wapinzani wetu, kila tutakayekutana naye hatutakuwa na huruma, kikubwa sasa ni kuendelea kulipa sapoti benchi la ufundi pamoja na wachezaji wetu ili kufikia malengo yetu," Popat aliongeza.

Azam FC itashuka dimbani tena kucheza mechi ya raundi ya nane Jumatatu kuwakabili wenyeji Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002